JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

TAARIFA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KWENYE MKUTANO WA KUMI NA NNE NA MKUTANO WA KUMI NA TANO PAMOJA NA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KUHUSU SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KWENYE MKUTANO WA KUMI NA MBILI NA MKUTANO WA KUMI NA TATU

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA

SEPTEMBA, 2024

IKISIRI

Taarifa hii inaripoti matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo na uchambuzi wa sheria ndogo. Taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge zinahusu hatua iliyofikiwa katika urekebishaji wa dosari za sheria ndogo zilizokuwa zimebainishwa kwenye sheria ndogo ambazo ziliwasilishwa mezani wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge. Uchambuzi wa sheria ndogo unagusa sheria ndogo **mia moja na sabini na tisa (179)** zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Kumi na Nne na sheria ndogo **mia moja na sitini na tatu (163)** zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge.

Kimuundo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu na sehemu ya kuhitimisha inayobainisha shukurani ikijumuisha kutoa hoja kwa ajili ya uamuzi wa Bunge. Sehemu ya kwanza inatoa malelezo ya jumla ambapo, lengo la Kamati kuripoti Bungeni na sababu za Bunge kufuatilia sheria ndogo vimefafafanuliwa. Katika sehemu hii, mambo **sita** yanayolengwa na utaratibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuripoti matokeo ya uchambuzi Bungeni yamefafanuliwa. Aidha, sababu **nne** za Bunge kufuatilia sheria ndogo zimeelezwa katika sehemu hii. Kadhalika, mbinu **saba** zilizotumika kufanikisha dhima ya Kamati zimebainishwa.

Sehemu ya Pili inaeleza shughuli za uchambuzi ambapo, shughuli ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge imeelezewa na shughuli za uchambuzi wa Sheria ndogo imefafanuliwa. Mantiki ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu dosari za sheria ndogo imebainishwa. Katika ufafanuzi imeelezwa kuwa Bunge linafuatilia taarifa za utekelezaji kutokana na umuhimu wa Bunge kufuatilia utekelezaji wa madaraka yake ya kuweka sheria za nchi. Shughuli zilizofanyika ni kupokea taarifa za utekelezaji na kufanya mapitio kwa lengo la kubaini iwapo marekebisho yamefanyika kadiri Bunge lilivyoazimia na hatua iliyofikiwa katika marekebisho hayo.

Kwa upande wa uchambuzi wa sheria ndogo, vimetajwa vipimo **vitano** vilivyotumika. Vipimo hivyo ni iwapo: sheria ndogo zina masharti yanayokizana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; sheria ndogo zina masharti yanyokinzana na sheria mama au sheria nyiongine za nchi; Sheria ndogo zina dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa

sheria; Sheria ndogo zina masharti yasiyo na uhalisia; na sheria ndogo zina dosari za kiuandishi wa majedwali.

Matokeo ya uchambuzi yamebainishwa ambapo, sheria ndogo mbili (02) zimebainika kuwa na dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Sheria ndogo kumi (10) zimebainika kuwa na dosari ya kuwa na vifungu vinavyoikinzana na sheria mama au sheria nyingine za Bunge; Sheria ndogo ishirini na mbili (22) zimebainika kuweka masharti yasiyo na uhalisia; Sheria ndogo kumi na tatu (13) zimebainika kuwa na dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria; na sheria ndogo kumi na tatu (13) ambazo zina dosari za uandishi wa majedwali. Ufafanuzi wa matokeo hayo umefanyika kwa kurejea Jedwali la uchambuzi na mifano halisi imetumika kuelezea dosari zilizobainika.

Sheria ndogo tano zenye dosari zimetumika kuwa mifano katika ufafanuzi. Sheria ndogo hizo ni: Sheria ndogo ya (Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 (TS Na. 38/19 Januari, 2024); Sheria ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 (TS Na. 920 22 Disemba, 2023); Sheria ndogo ya Usafi, Afya na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, 2023 (TS Na. 921/22 Disemba, 2023); Sheria ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, 2024 (TS Na. 30 la 12 Januari, 2024) na Regulations under The Atomic Energy (Protection from Ionizing and Non - Ionizing Radiation), 2023 (TS Na. 840/ 17 Novemba, 2023).

Sehemu ya tatu ya taarifa hii imebainisha maoni na mapendekezo kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi. Maoni yametolewa kwa mambo **sita** kuhusu dosari zilizobainishwa. Jambo la kwanza linahusu dosari ya sheria ndogo kukinzana na masharti ya Katiba, ambapo Kamati imetoa maoni kwamba, dosari hiyo inaathiri uthabiti wa mfumo wa sheria za nchi na kwamba ina madhara makubwa katika utekelezaji. Jambo la pili linahusu dosari ya sheria ndogo kuwa na masharti yanayokinzana na sheria mama. Katika hili, Kamati ina maoni kwamba, dosari hiyo inaweza kukwamisha azma ya sheria mama au sheria nyingine ya Bunge na kwamba, haikuwa lengo la Bunge kukwamisha azma ya sheria mama wakati lilipokasimu madaraka ya kuweka sheria ndogo. Jambo la tatu linahusu dosari ya sheria ndogo kuweka masharti yasiyo na uhalisia. Dosari hii inathiri

utakelezaji wa malengo yaliyokusidiwa pia kutatiza utekelezaji wake miongoni mwa wasimamizi wa sheria inayohusika.

Jambo la nne lilihusu dosari ya sheria ndogo kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria. Kwa dosari hiyo, Kamati imetoa maoni kwamba, inaathiri ubora kwenye ufasaha, usahihi, ukamilifu na kueleweka kwa sheria inayohusika. Jambo la tano lilihusu dosari ya sheria ndogo kuwa na majedwali yenye kasoro za kiuandishi wa majedwali. Kwa maoni ya Kamati dosari hii inaathiri ufafanuzi uliokusudiwa kufanyika kwa kutumia jedwali. Hivyo, Kamati ina maoni kuwa dosari hiyo isiporekebishwa itaendelea kukwamisha utekelezaji wa sheria ndogo zinazohusika.

Kwa msingi wa maoni ya Kamati yaliyobainishwa katika sehemu ya tatu ya taarifa, Kamati imependekeza yafuatayo: -

(i) Mamlaka zilizotunga sheria ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 01** cha Taarifa hii, zirekebishe dosari za sheria ndogo zinazohusika;

(ii) Mamlaka zilizotunga sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi kama ilivyobainishwa katika **Kiambatisho Na. 01** cha Taarifa hii, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hiyo;

(iii) Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na dosari ya kuweka masharti yasiyo na uhalisia kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 01**, zirekebishe dosari hiyo ili kufikia malengo yoliyokusudiwa;

(iv) Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 01**, zirekebishe dosari hiyo ili kuleta tija iliyokusudiwa;

(v) Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zilibainika kuwa na majedwali yenye dosari za kiuandishi kama inavyobainishwa kwenye **Kiambatisho Na. 01**, zifanye marekebisho ili kuepusha madhara ya dosari zilizobainika;

(vi) Mamlaka zote zinazohusika na sheria ndogo zenye dosari kama zilivyotajwa katika **Kiambatisho Na. 01** cha Taarifa hii, ziwasilishe Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio yote Kuhusu Dosari za Sheria

Ndogo kwa Katibu wa Bunge, ifikapo ifikapo saa tisa na nusu ya tarehe 20 Disemba, 2024; na

(vii) Mamlaka ambazo hazijakamilisha utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, zikamilishe mchakato wa marekebisho na kwamba, ifikapo saa tisa na nusu ya tarehe 27 Septemba, 2024 ziwe zimewasilisha kwa Katibu wa Bunge, taarifa za utekelezaji wake zenye ushahidi wa kurekebishwa kwa dosari zilizobainika katika sheria ndogo zinazohusika.

YALIYOMO

IKISIRI.....i

YALIYOMO..... v

MUHTASARI WA UFAFANUZI WA SEHEMU KUU ZA TAARIFA vii

SEHEMU YA KWANZA 1

1.0 UTANGULIZI..... 1

1.1 Maelezo ya Jumla 1

1.2 Muundo wa Taarifa 1

1.3 Lengo la Kamati Kuripoti Bungeni kuhusu Sheria Ndogo 2

1.4 Sababu za Bunge Kufuatilia Sheria Ndogo 3

1.5 Mbinu Zilizotumika Kupata Matokeo 5

1.6 Majumuisho ya Sehemu ya Kwanza..... 6

SEHEMU YA PILI..... 8

2.0 SHUGHULI ZA UCHAMBUZI..... 8

2.1 Maelezo ya Jumla 8

2.2 Msingi wa Shughuli za Uchambuzi 9

2.2.1 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo..... 10

2.2.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano 12

2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo..... 14

2.3.1 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho Kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki..... 19

2.3.2 Hatua ya Marekebisho Kutangazwa katika Gazeti la Serikali 20

2.4 Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano 24

2.4.1 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Katiba..... 25

2.4.2 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi..... 26

2.4.3 Dosari ya kuweka Masharti yasiyo na Uhalisia 28

2.4.4 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria29

2.4.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali 30
2.5 Majumuisho ya Sehemu ya Pili 32
SEHEMU YA TATU 33
3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO 33
3.1 Maelezo ya Jumla 33
3.2 Maoni 33
3.3 Mapendekezo 34
3.3.1 Sheria Ndogo kuwa na Masharti yanayokinzana na Masharti ya Katiba 35
3.3.2 Dosari ya kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi 35
3.3.3 Dosari ya Kuweka Masharti yasiyo na Uhalisia 36
3.3.4 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria37
3.3.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali 38
3.3.6 Kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio kuhusu Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na Dosari 38
3.3.7 Kutokamilika kwa Utekelezaji wa Maazimio ya Kurekebisha Sheria Ndogo 39
3.4 Majumuisho ya Sehemu ya Tatu 40
SEHEMU YA NNE 41
4.0 HITIMISHO 41
4.1 Shukrani 41
4.2 Hoja 43

MUHTASARI WA UFAFANUZI WA SEHEMU KUU ZA TAARIFA

SEHEMU	MUKTADHA WA UCHAMBUZI	KIPENGELE CHA MSINGI	KIGEZO KILICHOZINGATIWA
Sehemu ya kwanza	Uzingatiaji wa Masharti ya Kifungu cha 10 (1) – 10(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023	(i) Mtiririko unaoonekana kwenye muundo wa taarifa (ii) Sababu za Bunge kufuatilia Sheria Ndogo (iii) Sababu za Kamati kuripoti Bungeni matokeo ya uchjambuzi wa sheria ndogo	Mashari ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge kuhusu Muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayoingia Bungeni
Sehemu ya Pili	Mamlaka ya kuweka sheria za nchi ni Bunge na wananchi wanaowakilishwa Bungeni wanastahili kuwa na ustawi unaowekewa	(i) Ufafanuzi wa shughuli za uchambuzi (ii) Matokeo ya uchambuzi yanayoonesha hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge na dosari zilizobainika katika sheria ndogo zilizochambuliwa	Masharti ya Kifungu cha 10 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kwa kujiridhisha Iwapo sheria ndogo – (i) zina masharti yanayokinzana na Katiba; (ii) zina masharti yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria nyingine za

SEHEMU	MUKTADHA WA UCHAMBUZI	KIPENGELE CHA MSINGI	KIGEZO KILICHOZINGATIWA
			nchi; (iii) zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi; (iv) zina masharti yasiyo na uhalisia kwa kiasi cha kusababisha changamoto katika utekelezaji wake; na (v) zina majedwali yenye dosari za kiuandishi.
Sehemu ya Tatu	Maoni ya Kamati kuhusu mambo sita (06) yanayotokana na uchambuzi na mapendekezo saba (07) yanayolenga kurekebishwa kwa dosari zilizobainika katika sheria ndogo.	Maoni ya Kamati na Mapendekezo yanayotolewa yanatokana na nafasi ya Bunge katika sheria za nchi, uhusiano wa Bunge na Wananchi, lengo kuu la Serikali kwa mujibu wa Katiba na matarajio ya Wananchi.	Masharti ya (i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano (ii) Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na (iii) Kanuni za Bunge

SEHEMU	MUKTADHA WA UCHAMBUZI	KIPENGELE CHA MSINGI	KIGEZO KILICHOZINGATIWA
Sehemu ya Nne	Shukurani na Utoaji wa hoja ili Taarifa ya uchambuzi unaohusu sheria ndogo ijadiliwe na kuamuliwa na chombo chenye mamlaka kuu ya kuweka sheria za nchi.	(i) Shukurani kwa Mhe. Spika na Katibu wa Bunge (ii) Shukurani kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (iii) Shukurani kwa Mawaziri waliofika kwenye Kamati (iv) Ombi kwa Bunge kupitisha mapendekezo kuwa Maazimio ya Bunge	(i) Kanuni ya 61 (1) ya Kanuni za Bunge inayohusu kutoa pendekezo linalokamilika ili kupata uamuzi wa Bunge (ii) Bunge ni Mamlaka kuu ya Utungaji wa Sheria na linaweza kukasimu madaraka yake ambapo si kung'atuka katika madaraka ya Bunge kuweka sheria za nchi

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo naomba kuwasilisha Taarifa ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowekwa mezani wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge. Taarifa hii inajumuisha uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowekwa Mezani wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kuona umuhimu wa kuiweka Taarifa hii kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge (Order paper) ya leo, kwa mamlaka uliyonayo kwa mujibu wa Kifungu cha 10 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Bila shaka uamuzi huu umetokana na uongozi wako mahiri na azma yako madhubuti ya kuliwezesha Bunge kutimiza wajibu wake wa kusimamia misingi ya kidemokrasia kupitia usimamizi wa madaraka ya kuweka na Sheria Ndogo katika mfumo wa Sheria. Bunge ambalo ni chombo muhimu cha kidemokrasia linajivunia uongozi wako adhimu hususani katika kusimamia madaraka maalumu ya Bunge yanayohusu sheria za nchi.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 42 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hivyo, unaendana na matarajio ya Bunge kwa Kamati ili liweze kutekeleza madaraka yake ipasavyo. Kwa madhumuni ya kurahisisha mtiririko na ufuatiliaji, naomba kutambulisha sehemu hizo za Taarifa hii ambayo

imegawanyika katika sehemu kuu tatu na ya nne ni kutoa hoja na shukurani. Sehemu hizo ni ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inayohusu utangulizi inaonesha maelezo ya jumla kuhusu taarifa yenyewe, lengo la Kamati kuripoti Bungeni, mantiki ya Bunge kufuatilia Sheria Ndogo na mambo mengine ya jumla kuhusu Taarifa ya Kamati;

(ii) Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi inabainisha shughuli za uchambuzi na misingi yake pamoja na matokeo ya uchambuzi. Katika sehemu hii sheria ndogo zilizochambuliwa na vigezo vya uchambuzi ni mambo yanayofafanuliwa.

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni ya Kamati kuhusu Matokeo ya Uchambuzi pamoja na kutoa Mapendekezo ili Bunge likiyapitisha yawe maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, muundo huo utawezesha wafuatiliaji kubaini mzizi wa mapendekezo na muktadha wake. Waheshimiwa Wabunge wataona dhahiri kila pendekezo linavyofaa kuungwa mkono kwa lengo la kufanikisha dhima ya Bunge kuwa na sheria bora za nchi.

1.3 Lengo la Kamati Kuripoti Bungeni kuhusu Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kama ilivyo kwa Kamati nyingine za Bunge, inafanya kazi kwa niaba ya Bunge na kwa kutumwa na Bunge. Matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo na uamuzi stahiki kwa matokeo hayo ni stahili ya Bunge kuamua kwa njia ya maazimio. Ili kufanikisha jambo hilo, taarifa hii inalenga kuliwezesha Bunge lifanikiwe katika mambo yafuatayo: -

(i) Kupata tathmini ya jumla na ya kina inayochangiwa na Wabunge kwa ujumla ili kuwa na uelewa na msimamo wa

pamoja kuhusu madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali za kiutendaji;

(ii) Kuwezesha ulingo (*forum*) muhimu unaoruhusu mitazamo tofauti (*diverse perspectives*) ya Wabunge ili nchi iwe na Sheria zinazokidhi matarajio ya wananchi;

(iii) Kujenga makubaliano ndani ya Bunge kuhusu hatua stahiki kulingana na uhalisia wa sheria ndogo zilizofanyiwa uchambuzi;

(iv) Kutumia mchakato wa kidemokrasia na kuwezesha uwazi kwa njia ya mjadala Bungeni unaotoa nafasi kwa Wabunge kuongeza maoni yao katika matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo;

(v) Kuzingatia dhana ya uwajibikaji kwa umma (*Public Accountability*) kwa kuuwezesha Umma kufuatilia kiwango cha umakini unaojitokeza kwenye uchambuzi wa sheria ndogo zinazogusa moja kwa moja maisha ya wananchi; na

(vi) Kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa mapendekezo yanayolenga kuondosha dosari za sheria ndogo, kutokana na uchangiaji wa Wabunge unaoongezea ufafanuzi kwa watekelezaji.

1.4 Sababu za Bunge Kufuatilia Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyofahamu, Bunge ndilo lenye mamlaka ya kutunga Sheria zote za nchi. Hivyo, ubaya au uzuri wa sheria za nchi unabebwa na Bunge. Iwe sheria mama au sheria Ndogo, matokeo yake kwa maisha ya watu ni dhima ya Bunge. Aidha, Ibara 8 (1) (a) inasisitiza kuwa wananchi ndio msingi wa mamlaka yote.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano imeelekeza lengo kuu la Serikali ambalo ni ustawi wa watu. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linapaswa kuhakikisha kuwa sheria ndogo zote kama ilivyo kwa Sheria za Bunge, haziweki ugumu wa kupata maisha bora wala hazizalishi kero kwa wananchi ambao ni msingi wa mamlaka yote ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, Bunge kupitia Kamati yake ya Sheria Ndogo linafuatilia sheria ndogo kwa sababu kuu zifuatazo: -

(i) Kudumisha ukuu wa watu (*People's sovereignity*) kwa kuhakikisha kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kuweka sheria ndogo hazizidi mamlaka ya utungaji sheria yaliyotolewa na watu kwa wawakilishi wao (Bunge);

(ii) Kuhakikisha kwamba, madaraka ya kuweka sheria ndogo katika mfumo wa sheria za nchi, yaliyokasimiwa na Bunge kwa mamlaka mbalimbali hayavunji haki za watu na wala hayavuki mipaka;

(iii) Kuzuia masuala ya kiufundi na utaalamu yasivuke mipaka na kuathiri maisha ya watu au kuvuruga haki na usawa miongoni mwa watu; na

(iv) Kuhakikisha kwamba Sheria zinazotokana na Bunge kukasimu madaraka yake, zinaakisi maslahi ya umma kwa upana wake, maadili ya jamii pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya ustawi wa watu.

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huo, Bunge hili linatarajiwa kujadili ipasavyo Taarifa hii na kutoa maazimio yanayolenga kuondosha dosari zilizobainika katika sheria ndogo. Kwa msingi huo, Kamati imefanya uchambuzi wa kina, imekuwa makini na imeweka

wazi matokeo ya uchambuzi katika Jedwali la kwanza ambalo ni **Kiambatisho Na. 01** na Jedwali la pili la matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa maazimio ya Bunge ambalo ni **Kiambatisho Na. 02.** Majedwali yote hayo ni sehemu ya Taarifa hii na yameambatishwa.

1.5 Mbinu Zilizotumika Kupata Matokeo

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa mbinu inayotumiwa na Kamati, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, imeweka masharti kwamba, kila Taarifa inayowasilishwa Bungeni itabainisha njia iliyotumika. Kwa kawaida, njia iliyotumika inapobainishwa kwenye taarifa ya Kamati Bungeni, inasaidia mambo yafuatayo: -

(i) Kuweka wazi muktadha wa matokeo ya uchambuzi na hivyo kujenga msingi wa uhalali wa matokeo yanayowasilishwa Bungeni;

(ii) Kuweka uwazi wa vigezo na mchakato uliotumika na hivyo kulisaidia Bunge tathmini ya uhalali wa mapendekezo yanayotolewa;

(iii) Kuwezesha tathmini ya ubora wa matokeo yanayoripotiwa Bungeni kulingana na ubora wa njia na hivyo kuwezesha tathmini ya msingi wa mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kuonesha njia katika Taarifa za Kamati ni jambo linawezesha Bunge kujiridhisha na kiwango cha kazi iliyofanywa na Kamati. Kwa mantiki hiyo, naomba kubainisha mbinu zilizotumika ambazo ni: -

(i) Kupitia Magazeti ya Serikali yaliyotangaza sheria ndogo na kuwekwa mezani Bungeni;

(ii) Kubainisha sheria ndogo zinazofaa kujadiliwa kwa kipaumbele na kufanya mapitio ya sheria ndogo hizo;

(iii) Kubainisha sheria ndogo zenye hoja za kiuchambuzi na kuzipitia kwa undani ili kufanya tathmini kwa umakini Zaidi;

(iv) Kusoma matini (*text*) ya sheria ndogo na matini ya sheria mama kwa lengo la kuoanisha masharti ya kisheria;

(v) Kuchunguza dhamira ya sheria mama ili kujiridhisha iwapo sheria ndogo zinaendana na nia ya Bunge;

(vi) Kutafakari dhamira ya sheria ndogo inayohusika kwa kulinganisha na nia ya Bunge kukasimu madaraka yake kwa mamlaka inayohusika;

(vii) Kutathmini sheria ndogo kwa muono wa miongozo ya uandishi wa sheria iliyotolewa katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1; na

(viii) Kufungamanisha Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba inayobainisha lengo kuu la Serikali kwa upande mmoja na maudhui, dhamira na masharti ya Sheria Ndogo kwa upande mwingine ili kutathmini kwa vigezo vya uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, nilithibitishie Bunge lako tukufu kuwa matumizi ya mbinu hizo, yamefanikisha matokeo ya uchambuzi. Naamini Bunge likijadili ipasavyo, uchambuzi uliofanyika utakuwa na tija kwa maisha ya Watanzania. Naomba kusisitiza kwamba, Wabunge na wananchi tukumbuke vizuri kuwa, sheria ndogo zilizochambuliwa na matokeo yake kuripotiwa, kwa sehemu kubwa zinagusa maisha ya kawaida na ya kila siku ya wananchi. Hivyo, ni muhimu kufuatiliwa kwa umakini.

1.6 Majumuisho ya Sehemu ya Kwanza

Mheshimiwa Spika, maelezo yanayotolewa katika sehemu ya kwanza yanaweka muktadha wa Taarifa. Katika maelezo hayo muundo wa taarifa na msingi wake umebainishwa ili kuonesha

mtiririko wa maudhui. Aidha, lengo la Kamati kuripoti Bungeni limewekwa bayana ili kuwezesha ufuatiliaji wa mambo makuu katika taarifa. Vilevile, sababu za Bunge kufuatilia sheria ndogo zimedhihirishwa ili kuonesha mantiki ya taarifa. Zaidi ya hivyo, sababu za Bunge kufuatilia sheria ndogo zimebainishwa ili kushajiisha mjadala wa taarifa hii. Pia zimeelezwa mbinu zilizotumika kwa lengo la kuwezesha tathimini ya matokeo yanayoripotiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla jambo kuu la kuondoka nalo katika sehemu hii ni madhumuni ya taarifa ya Kamati Bungeni. Imeelezwa kwamba, Bunge ndilo lenye mamlaka ya kutunga sheria na ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi. Hivyo, linategemewa kuhakikisha kuwa sheria zote za nchi zinawezesha ustawi wa maisha yao kuliko kuwa kero kwao. Aidha, Bunge kwa utaratibu wake linategemea matokeo ya kazi ya Kamati hii kuona kuwa kuna taratibu bora za utekelezaji wa sheria. Jambo lingine muhimu ni kuzingatia dhima ya Bunge ambayo inaliweka Bunge kwenye kuhusika na ubaya au uzuri wa sheria za nchi. Ikumbukwe kuwa wananchi hawatarajii Bunge liache dosari za sheria yoyote ya nchi iwe kikwazo kwa ustawi wao.

SEHEMU YA PILI

2.0 SHUGHULI ZA UCHAMBUZI

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati hii inategemewa na Bunge katika azma yake ya kuhakikisha sheria za nchi zinajali ustawi wa wananchi, Taarifa hii ni zana ya msingi kutimiza azma ya Bunge. Kwa kuwa Bunge ni mamlaka kamili ya kutunga sheria kwa mujibu wa Katiba, halipaswi kung'atuka katika utungaji wa sheria ndogo. Badala yake, Bunge linapokasimu madaraka yanayohusika, linapaswa kufuatilia kwa kuchambua sheria ndogo na kutoa maazimio kutokana na uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo inahakikisha kuwa Bunge linapokasimu sehemu ya madaraka yake ya kutunga sheria, haling'atuki. Kamati imefanya hivyo kwa shughuli zake kuu mbili zifuatazo: -

(i) Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano. Lengo ni kuhakikisha kuwa dhima ya Bunge inabaki kama ilivyo na inavyotarajiwa kusaidia nchi kuwa na sheria za nchi zinazostahili; na

(ii) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu. Lengo ni kusimamia uzingatiaji wa madaraka ya Bunge ya kutunga sheria na kuhakikisha kuwa Bunge linayatawala madaraka hayo yasiyotakiwa kutelekezwa.

2.2 Msingi wa Shughuli za Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Msingi mkuu wa shughuli za uchambuzi umejengwa kwenye Ibara ya 4 (1), Ibara ya 8 (1(a) na (1)(b) na Ibara ya 97 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, masharti na lengo la jumla la Sheria ya Taafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The interpretation of Laws Act, Cap.* 1) kwa pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge, yanazatiti umuhimu wa shughuli za uchambuzi zilizofanywa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 (1) ya Katiba imelipatia Bunge shughuli za mamlaka ya nchi zinazohusu kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Hivyo, katika nchi utungaji wa sheria zote upo chini ya mamlaka ya Bunge. Hata hivyo, Bunge linaruhusiwa kukabidhi kwa mtu yoyote au kwa Idara yoyote ya Serikali, madaraka ya kuweka Kanuni zenye nguvu ya kisheria au kuzipa nguvu ya kisheria Kanuni zozote zilizowekwa na mtu yoyote au Idara yoyote ya Serikali. Sheria na Kanuni kwa msingi huo, zinapaswa kuzingatia masharti ya Ibara ya 8 (1) (a) kwamba, Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na kwamba Serikali imepata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa Wananchi. Hivyo, sheria za nchi zinalazimika kuweka masharti yanayolinda na kuzingatia ipasavyo maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, ndiyo inayotoa mwongozo kuhusu uandishi wa sheria. Sheria hii ina lengo la kuzatiti sheria kwenye muundo wa uandishi. Aidha, inaweka mwongozo wa tafsiri na masharti kuhusu matumizi ya sheria zote. Hivyo, inajenga msingi wa uchambuzi ikiwemo kubainisha masharti ya sheria ndogo kuwekwa mezani Bungeni. Kwa masharti hayo, sheria hii kwa pamoja

na Kanuni za Kudumu za Bunge ni mwongozo wa msingi katika shughuli za uchambuzi zinazofanywa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kwa msingi niliioueleza hapo juu, Taarifa hii inafafanua shughuli za Kamati ambazo zinahusu uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge na Uchambuzi wa Sheria Ndogo.

2.2.1 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo **ishirini na mbili** (22) zilizowasilishwa Bungeni tarehe 5 Septemba, 2023, kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili na tarehe Tarehe 07 Novemba, 2023 kwenye Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge. Ufuatiliaji huo ulioambatana na upokeaji na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji, ulilenga kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa uamuzi wa Bunge kuhusu mamlaka yake ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Spika, mantiki ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio inatokana na umuhimu wa Bunge kutekeleza jukumu la kutunga sheria pasi na kusahau wajibu wake kikatiba kuhusu sheria za nchi ikiwemo sheria ndogo. Nilikumbushe Bunge lako tukufu kuwa, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo hizo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 16 Februari, 2024 kwenye Mkutano wa Kumi na Nne. Matokeo hayo yalihusu dosari mbalimbali na pia yalionesha madhara yake dhidi ya misingi ya sheria na ustawi wa watu uliosisitizwa katika Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio unalisaidia Bunge kufuatilia hatua mbalimbali zilizofikiwa ili kurekebisha dosari kwenye sheria ndogo. Kufanya hivyo ni muhimu na lazima kwa kuwa Bunge ndilo mamlaka kuu ya utungaji wa sheria za nchi. Hivyo, maoni ya Kamati kutokana na uchambuzi huo yanajenga msingi mzuri utakaowezesha mjadala na tathmini ya Bunge kuhusu namna madaraka yake yanavyotumiwa na mamlaka nyingine za serikali.

Mheshimiwa Spika, shughuli za uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge zilifanyika kwa hatua mbalimbali za Kamati. Hatua hizo zinaelezwa kama ifuatavyo: -

(a) Kupokea Taarifa za Utekelezaji kabla ya kukutana na Mamlaka Zilizohusika

Mheshimiwa Spika, kabla ya kukutana na mamlaka zilizoandaa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge, Kamati ilijiwekea utaratibu wa kuzichambua. Nia ni kuoanisha utekelezaji ikilinganishwa na maazimio yaliyopitishwa na Bunge. Kwa mantiki hiyo, hatua hii ilisaidia katika mambo makuu mawili yafuatayo: -

(i) Kutathmini iwapo kuna mkwamo au kusuasua katika hatua mbalimbali za utekelezaji; na

(ii) Kuoanisha hatua ya utekelezaji na madhara ya dosari yaliyonusurika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulithibitishia Bunge hili kuwa, mambo hayo mawili, yanasaidia kulionesha Bunge iwapo utekelezaji umeendana na matarajio yake. Hivyo, kuliweka

Bunge katika nafasi muhimu ya kutekeleza na kusimamia madaraka yake liliyoyakasimu kwa mamlaka nyingine serikalini.

(b) Kukutana na Mamlaka Zilizotakiwa Kutekeleza Maazimio ya Bunge

Mheshimiwa Spika, Baada ya kupokea taarifa za utekelezaji na kufanya mapitio ya jumla, Kamati ilikutana na mamlaka zinazohusika ili kujadiliana yaliyobainika katika taarifa hiyo. Lengo la hatua hii ni kuzingatia utaratibu mzuri wa misingi ya asili kisheria ili kufikia msimamo wa kutumainiwa juu ya jambo linalohusika. Aidha, hatua hii iliiwezesha Kamati kupata ufafanuzi wa kina kwa mbambo yaliyobainika baada ya mapitio ya taarifa.

2.2.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 2 Februari, 2024 wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Serikali iliwasilisha Mezani Bungeni matoleo ya Magazeti ya Serikali kumi na Mbili (12) yakiwa na jumla ya Sheria Ndogo **Mia moja Sabini na Tisa (179).** Aidha, tarehe 8 Aprili, 2024 katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, Serikali iliwasilisha Mezani jumla ya Magazeti Kumi yenye jumla ya sheria ndogo **Mia Moja Sitini na Tatu (163).**

Mheshimiwa Spika, baada ya sheria ndogo zinazohusika kuwasilishwa mezani, kwa mamlaka yako ulizileta kwenye karakana ya sheria ndogo ambayo ni Kamati hii inayoripoti leo Bungeni. Ni wazi kuwa madhumuni ya hatua yako ni kufanikisha azma ya Bunge kutunga sheria za nchi zenye misingi sahihi na

madhubuti zinazolenga kuangalia maslahi mapana ya wote wanaoguswa na sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa iliyofanyika kwenye Kamati ikiwa ni karakana ya sheria ndogo ni kubainisha hitilafu kwenye matumizi ya madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini. Shughuli hiyo ilijumuisha kuonesha dosari katika sheria ndogo na madhara yake kwa wananchi, sambamba na kupendekeza hatua stahiki ya kuchukuliwa na Bunge ili kusahihisha kasoro zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kipimo kikuu kilichotumika ni masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Kamati ililenga kujiridhisha na mambo makuu matano (05) yafuatayo: -

(a) Iwapo sheria ndogo zina masharti yanayokinzana na Katiba;

(b) Iwapo sheria ndogo zina masharti yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi;

(c) Iwapo sheria ndogo zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi;

(d) Iwapo sheria ndogo zina masharti yasiyo na uhalisia kwa kiasi cha kusababisha changamoto katika utekelezaji wake; na

(e) Iwapo sheria ndogo zina majedwali yenye dosari kwa -

(i) kutofautiana na vifungu vya sheria ndogo vinavyoyaanzisha au:

(ii) kutokamilika ilivyostahili au;

(iii) kutajwa katika sheria ndogo inayohusika lakini yanakosekana; na

(iv) kujitokeza bila kuwa na kifungu cha sheria ndogo inayoyaanzisha.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla shughuli za Kamati zililenga maeneo makuu mawili. Eneo la kwanza ni hatua zilizofikiwa katika marekebisho ya dosari za sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na tatu. Eneo la pili ni dosari katika sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na tano.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote hayo yanahusu madaraka ya Bunge kwenye sheria za nchi. Tathmini ya hatua iliyofikiwa katika maazimio ya Bunge ni muhimu ili kuhakikisha kuwa madaraka ya Bunge yametekelezwa inavyostahili. Kujiridhisha na sheria ndogo ni shughuli muhimu kwa kuwa Bunge linatarajiwa na wananchi kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakuwepo kwa namna isiyokiuka misingi muhimu ya sheria.

2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, Bunge lako linao wajibu wa kuhakikisha kwamba, madaraka yake ambayo yamekabidhiwa kwa mamlaka nyingine yanatumika inavyostahili. Wajibu huo unalitaka Bunge kutokuishia kutoa maazimio kuhusu urekebishwaji wa sheria ndogo bali pia kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake. Ili kutimiza wajibu huo ni jukumu la Bunge lenyewe kufuatilia ipasavyo namna madaraka hayo yanavyotumika. Kwa maneno mengine, Bunge halipaswi kuishia

kwenye kubainisha dosari katika sheria ndogo na kuamua kwa njia ya maazimio. Kwa kawaida, Bunge linapaswa kujiridhisha iwapo dosari hizo zimerekebishwa kwa namna ilivyoazimiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Bunge linaituma Kamati ya Sheria Ndogo kusimamia utekelezaji bora wa madaraka ya sheria ndogo yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine, Kamati hii inawajibika kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Lengo ni kuona hatua inayofikiwa na kulinganisha na hatua iliyostahili ili kulishauri Bunge uamuzi unaofaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria ndogo ni sehemu ya Sheria za nchi, dosari zinazojitokeza katika Sheria hizo, zinapaswa kufanyiwa kazi kwa utaratibu unaoendana na desturi za Bunge. Bila kufanya hivyo, madhara ya dosari zote yanavyoendelea yanaweza kuliweka Bunge kwenye kulaumiwa na wananchi. Bunge ambalo ni chombo halisi cha wananchi haliwezi kuacha kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake kuhusu dosari katika sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio uliangalia hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio hayo. Uangaliaji na ufuatiliaji wa hatua hizo za utekelezaji ulidadisi mambo yafuatayo: -

(i) Iwapo hakuna kabisa utekelezaji wa maazimio;

(ii) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya Rasimu ya marekebisho katika ngazi ya Wizara;

(iii) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya Rasimu ya marekebisho kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki; na

(iv) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, udadisi ulioegemea katika vigezo hivyo, uliiwezesha Kamati kutathmini hali ya utekelezaji wa kila azimio lililotolewa na Bunge na hatimaye kupata matokeo halisi ya hatua zilizofikiwa katika utekelezaji. Matokeo hayo yataliwezesha Bunge kuamua kuhusu hatua inayofuata.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu dosari za sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, yanafaa kuripotiwa. Nia ni kuonesha hatua iliyofikiwa ili kusahihisha dosari kama ilivyoamuliwa kupitia maazimio ya Bunge. Matokeo hayo yanaonesha kwamba, hatua zilizoripotiwa za kusahihisha dosari ili kutekeleza maazimio ya Bunge, zinagawanyika katika makundi makuu yafuatayo: -

(i) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki; na

(ii) Hatua ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kufafanua hatua hizo sambamba na kubainisha Wizara tisa (09) zinazohusika. Lengo la ufafanuzi huu ni kuliwezesha Bunge kubaini kiwango cha utekelezaji wa maazimio yake na kufanya uamuzi stahiki. Ili kuweka bayana wahusika wa utekelezaji wa maazimio, naomba kubainisha Wizara zinazohusika na utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo. Wizara hizo ni: -

(i) Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji iliyokuwa na sheria ndogo **moja** (01) iliyobainika kuwa dosari **mbili** (02);

(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu iliyokuwa na sheria ndogo **mbili** (02) zilizobainika kuwa na dosari **sita** (06);

(iii) Wizara ya Kilimo iliyokuwa na sheria ndogo **moja** (01) zilizobainika kuwa dosari **kumi na sita** (16);

(iv) Wizara ya Uchukuzi iliyokuwa na sheria ndogo **sita** (06) zilizobainika kuwa dosari **thelathini** (30);

(v) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliyokuwa na sheria ndogo **mbili** (02) zilizobainika kuwa dosari **kumi na mbili** (12);

(vi) Wizara ya Maji iliyokuwa na sheria ndogo **moja** (01) iliyobainika kuwa dosari **moja** (01);

(vii) Wizara ya Nishati iliyokuwa na sheria ndogo **tatu** (03) zilizobainika kuwa dosari **ishirini na nne** (24);

(viii) Wizara ya Fedha iliyokuwa na sheria ndogo **nne** (04) zilizobainika kuwa dosari **kumi na nane** (18); na

(ix) Wizara ya Viwanda na Biashara iliyokuwa na sheria ndogo **mbili** (02) zilizobainika kuwa dosari tisa (09).

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge inabainishwa katika Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu, ambalo ni **Kiambatisho Na. 02**. Jedwali hilo linafafanua hatua iliyofikiwa na kila Wizara. Pamoja na hivyo, kwa madhumuni ya kuweka mtiririko huo kwa ajili ya kuwezesha

majadiliano juu ya hoja hii, naomba kufafanua hatua hizo kama ifuatavyo:

(i) Maazimio ya Bunge kutokuwa yametekelezwa.

(ii) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho katika ngazi ya Wizara.

(iii) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki.

(iv) Hatua ya Marekebisho Kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yanayoripotiwa katika Taarifa hii yameonekana kuwa katika hatua mbili zilizofikiwa na Wizara na Taasisi mbalimbali katika kutekeleza Maazimio ya Bunge. Hatua hizo zinahusisha marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali na Rasimu ya Marekebisho ya sheria ndogo kuwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki ili kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Kimsingi hatua hizi ni za juu kabisa katika utekelezaji wa Maazimio Bunge na zinastahili kupongezwa, kwani Kamati ilijiridhisha kuwa hakuna Wizara au Taasisi ambayo haijaanza kabisa utekelezaji wala kuwa katika hatua ya Rasimu ya marekebisho iliyo katika ngazi ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge lako tukufu kufahamu kuhusu hatua za utekelezaji na hatimaye kufanya uamuzi sahihi kuhusu hoja zitakazoazimiwa kutokana na Taarifa hii, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu hatua zilizofikiwa.

2.3.1 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho Kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya sheria ndogo zote yanatarijwa kufikishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Uchambuzi umebainisha kwamba, hadi wakati Kamati ilipokutana na Wizara zinazohusika, ni **sheria ndogo tatu** (**03**) tu, zilizokuwa na hoja **ishirini na tisa** (**29**) kati ya sheria **ndogo ishirini na mbili** (**22**) zilizokuwa na hoja **thelathini na mbili (32)** zilifika hatua hii. Sheria ndogo hizo ni: -

(i) Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji na Usambazaji Umeme, 2023 **(TS Na. 452 la tarehe 7 Julai 2023)** zilizo chini ya Wizara ya Nishati ambazo zilizokuwa na jumla ya hoja 16;

(ii) Kanuni za Ukusanyaji na Uchakataji wa Taarifa Binafsi,2023 **(TS Na. 349 la tarehe 12 Mei 2023)** ambazo zinasimamiwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zikiwa na hoja sita (06); na

(iii) *The Accountants and Auditors (Training and Examinations) By Laws, 2023* **(TS Na. 486 la terehe 21 Julai 2023)** zilizo chini ya Wizara ya Fedha zenye hoja saba (07).

Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa inakaribia kutangazwa kwa marekebisho katika Gazeti la Serikali. Kwa maelezo yaliyowasilishwa kwenye Kamati marekebisho yatakamilika katika kipindi kifupi kijacho. Itakapofika hatua hiyo, changamoto zilizobainika na kero miongoni mwa wanaolengwa na sheria ndogo zitakuwa zimetatuliwa.

2.3.2 Hatua ya Marekebisho Kutangazwa katika Gazeti la Serikali

Mheshimiwa Spika, marekebisho yoyote ya sheria ndogo hayawezi kuanza kutekelezwa kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Tathmini iliyofanywa na Kamati imeonesha kwamba, hadi tarehe 23 Agosti, 2024, sheria ndogo **kumi na tisa (19)** zilikua zimefikia hatua ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Naomba kuzitambua Wizara zinazohusika na sheria ndogo hizo kama ifuatavyo: -

(a) Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji iliyotangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 83 la tarehe 9/2/2024 imefanya marekebisho ya hoja mbili (02) kupitia The *Tanzania Investment (Amendment) Regulations*, 2024;

(b) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliyotangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 407 la tarehe 24/5/2024 hoja sita (06) kwenye Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Taratibu za Kushughulikia Malalamiko ya Ukiukwaji wa Misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi za Mwaka 2024;

(c) Wizara ya Kilimo iliyotangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 344 la tarehe 3/5/2024 jumla ya hoja kumi na sita (16) kwenye *The Plant Health (Amendment) Regulations, 2024;*

(d) Wizara ya Nishati iliyotangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali sheria ndogo mbili (02) ambazo ni: -

(i) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Usuluhishi wa Migogoro Itokanayo na Shughuli za Mkondo wa Juu Wa

Petroli za Mwaka 2024, iliyorekebisha kasoro tatu (03) kupitia Tangazo la Serikali Na. 643 la Tarehe 26/7/ 2024; na

(ii) *The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Internal Review Procedure) (Amendment) Rules, 2024* iliyorekebisha hoja tano (05) kupitia Tangazo la Serikali Na. 643 la Tarehe 26/7/ 2024.

(e) Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu iliyotangaza marekebisho ya sheria ndogo mbili (02) katika Gazeti la Serikali. Sheria hizo ni: -

(i) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Mazingira ya Kazi za Mwaka, 2024 iliyorekebisha hoja tatu (03) kupitia Tangazo la Serikali Na. 24 la Tarehe 16/8/2024; na

(ii) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Egonomia za Mwaka, 2024 iliyorekebisha hoja tatu (03) kupitia Tangazo la Serikali Na. 25 la Tarehe 16/8/2024.

(f) Wizara ya Viwanda na Biashara iliyotangaza marekebisho ya sheria ndogo mbili (02) katika Gazeti la Serikali. Sheria hizo ni: -

(i) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Utoaji wa Leseni za Biashara za Mwaka 2024 iliyorekebisha hoja saba (07) kupitia Tangazo la Serikali Na. 147 la Tarehe 8/3/2024; na

(ii) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Umiliki Manufaa za Mwaka 2024 iliyorekebisha hoja mbili (02) kupitia Tangazo la Serikali Na. 148 la Tarehe 8/3/2024.

(g) Wizara ya Fedha iliyotangaza marekebisho ya sheria ndogo tatu (03) katika Gazeti la Serikali. Sheria ndogo zinazohusika ni: -

(i) *The Foreign Exchange (Bureau De Change) (Amendment) Regulations, 2024* iliyorekebisha hoja nne (04) kupitia Tangazo la Serikali Na. 417 la tarehe 31/5/2024;

(ii) *The Banking and Financial Instiotutions (Prompts Corrective Actions) (Amendment) Regulations, 2024* iliyorekebisha hoja mbili (02) kupitia Tangazo la Serikali Na. 148 la Tarehe 31/5/2024; na

(iii) *The Capital Markets and Securities Tribunal (Amendment) Rules, 2024* iliyorekebisha hoja tano (05) kupitia Tangazo la Serikali Na. 468 la tarehe 14/6/2024.

(h) Wizara ya Uchukuzi iliyotangaza marekebisho ya sheria ndogo sita (06) katika Gazeti la Serikali. Sheria hizo ni: -

(i) *The Tanzania Shipping Agencies (Cargo Security and Safety of Terminal Operations) (Amendment) Regulations, 2024* imerekebisha hoja tisa (09) kupitia Tangazo la Serikali Na. 394 la tarehe 24/5/2024;

(ii) *The Merchant Shipping (Establishment and Operation of Aids to Navigation) (Amendment) Regulations, 2024* imerekebisha hoja nne (04) kupitia Tangazo la Serikali Na. 395 la tarehe 24/5/2024;

(iii) *The Merchant Shipping (Medical Examinations) (Amendment) Regulations, 2024* imerekebisha hoja mbili

(02) kupitia Tangazo la Serikali Na. 396 la tarehe 24/5/2024;

(iv) *The Tanzania Shipping Agencies (Shippers Registration) (Amendment) Regulations, 2024* imerekebisha hoja kumi (10) kupitia Tangazo la Serikali Na. 397 la tarehe 24/5/2024;

(v) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Ulinzi wa Mizigo na Usalama wa Shughuli za Kibandari za Mwaka 2024 imerekebisha hoja nne (04) kupitia Tangazo la Serikali Na. 406 la tarehe 24/5/2024; na

(vi) Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Usajili wa Wasafirishaji kwa Njia ya Maji za Mwaka 2024 imerekebisha hoja moja (01) kupitia Tangazo la Serikali Na. 408 la tarehe 24/5/2024.

(i) Wizara ya Maji iliyotangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 392 la tarehe 24/5/2024 hoja moja (01) kwenye Kanuni za *The Water Supply and Sanitation (Commercial and Community Boreholes Operations) (Amendment) Rules, 2024*.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hatua kuu mbili zilizofikiwa ni sehemu ya juhudi za kurekebisha dosari zilizokuwa zimejitokeza kwenye sheria ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge. Kwa juhudi hizo, ni jambo jema kuanza mchakato wa kuondoa madhara ya dosari kama ilivyoazimiwa na Bunge. Hata hivyo, ni muhimu kwa mamlaka zinazokasimiwa na Bunge madaraka ya kuweka sheria ndogo, kufanya marekebisho kwa wakati pale ambapo, chombo kikuu

chenye mamlaka kuhusu sheria za nchi kinapoazimia kufanyika kwa marekebisho. Haifai kuchelewa kutekeleza maazimio ya Bunge hususan yanayolenga kurekebisha dosari katika sheria ndogo.

2.4 Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, yanaonesha dosari mablimbali kama inavyoenekana katika **Kiambatisho Na.1**. Naomba Jedwali hilo lisomwe kwa pamoja na taarifa hii na liingizwa kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Dosari zinazobainishwa katika Jedwali hilo zinajitokeza kwenye sheria ndogo zaidi ya moja. Kwa msingi huo, idadi ya dosari haitalingana na jumla ya idadi ya sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa idadi ya Sheria ndogo kulingana na aina ya dosari unaoesha kategoria zifuatazo: -

(i) Sheria ndogo mbili (02) zina masharti yanayokinzana na Katiba;

(ii) Sheria ndogo kumi (10) zina masharti yanayokinzana na Sheria Mama na sheria nyingine za nchi;

(iii) Sheria ndogo ishirini na mbili (22) zina masharti yasiyo na uhalisia

(iv) Sheria ndogo kumi na tatu (13) zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi; na

(v) Sheria ndogo kumi na tatu (13) zina dosari katika Majedwali.

Mheshimiwa Spika, Ili kuliwezesha Bunge kufikia uamuzi unaostahili, sehemu hii inafafanua dosari zilizotajwa hapo juu kwa mifano halisi

kama ilivyobainika wakati wa uchambuzi. Ufafanuzi huo ni kama ifuatavyo: -

2.4.1 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Katiba

Mheshimiwa Spika, Nia ya sheria ndogo ni kufanikisha lengo kuu la sheria mama inayotungwa na Bunge. Aidha, sheria ndogo kama zilivyo sheria nyingine za nchi, zinatarajiwa kuendana na masharti ya Katiba ambayo ni msingi mkuu wa sheria za nchi zikiwemo sheria mama. Hata hivyo, uchambuzi unabainisha baadhi ya sheria ndogo zenye maudhui yanayotofautiana na matakwa ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa sheria ndogo zenye dosari hiyo ni **Sheria Ndogo ya (Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 (TS Na. 38/19 Januari, 2024)**. Kifungu cha 26 cha sheria ndogo hii kinataja makosa mbalimbali yanayokatazwa, ikiwemo kosa kwa mtu yeyote kufanya shughuli za kisiasa ikiwa ni pamoja na kupandisha bendera ya Chama cha Siasa. Katazo hilo limewekwa pasipo kufafanua maeneo yanayoguswa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna katazo hilo lilivyowekwa, inaweza kutafsirika kwamba, watu wote wanakatazwa kufanya shughuli za kisiasa, jambo ambalo ni kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, sheria ndogo kuwa na masharti yasiyoendana na Katiba kama ilivyo kwa sheria ndogo hii, ni dosari kubwa katika sheria za nchi. Madhara yake ni pamoja na sheria inayohusika kutokuwa halali, kukiuka misingi ya utawala wa shera na kuathiri vibaya masharti ya misingi ya

demokrasia nchini. Njia pekee ya kusahihisha dosari hiyo ni kuirekebisha sheria ndogo iliyobainika kuwa na dosari.

2.4.2 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi

Mheshimiwa Spika, Kama tunavyofahamu, sheria ndogo zinatokana na mamlaka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa sheria mama iliyotungwa na Bunge. Hivyo, katika hali ya kawaida sheria ndogo hazitarajiwi kukiuka masharti ya sheria ambayo inaipa nguvu. Kwa msingi huo, ikiwa sheria ndogo yoyote itakuwa na maudhui yanayokinzana na yale ya sheria mama, itakuwa imejipa nguvu isiyotokana na ithibati ya mamlaka yoyote.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya maelezo hayo, uandishi wa sheria za nchi ni zao la misingi iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria. Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinakataza sheria ndogo kukinzana na sheria mama au sheria nyingine ya nchi. Vilevile, kifungu hicho kinabatilisha sheria ndogo inayokinzana na masharti ya sheria mama au ya sheria nyingine ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Licha ya masharti hayo ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, uchambuzi umeonesha kuwa, zipo sheria ndogo zilizochambuliwa ambazo zina dosari ya kukinzana na sheria mama. Mfano wa sheria ndogo hizo ni **Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 (TS Na. 920 22 Disemba, 2023).** Kifungu cha 16 (e) cha sheria ndogo hii kinaweka katazo kwa mtu yeyote aliye ndani ya gari

kudondosha taka ngumu nje ya gari likiwa ndani au nje ya kituo cha magari na sehemu yoyote ile ambapo gari hilo linapita.

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo hii imekataza utupaji wa taka ngumu peke yake bila kujumuisha taka laini na nyinginezo. Kutokutajwa kwa taka laini na nyinginezo kunaweza kutafsirika kuwa ni ruhusu ya kutupa taka hizo. Tafsiri hiyo, inaathiri vibaya lengo la sheria ndogo na utekelezaji wa Sheria ya Bunge ambayo ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, hususan kufikiwa kwa lengo la kuweka mazingira kwenye hali ya usafi na usalama.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine wa sheria ndogo iliyobainika kuweka masharti yanayokinzana na sheria nyingine za nchi ni **Sheria Ndogo ya Usafi, Afya na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, 2023 (TS Na. 921/22 Disemba, 2023)**. Kifungu cha 3 cha sheria ndogo hii kinatafsiri maneno mbalimbali yaliyotumika katika sheria ndogo ikiwemo kifungu cha maneno "**taka ngumu**. Tafsiri hiyo inatofautiana na tafsiri ya "**taka ngumu** katika Kifungu cha 3 Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Kwa kufanya hivyo, sheria ndogo inakinzana na sheria mama inayoweka utaratibu wa usimamizi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, Bunge linapokabidhi kwa mamlaka za serikali madaraka ya kuweka sheria ndogo au kanuni, halikusudii kuruhusu mamlaka hizo zitunge sheria ndogo zinazokinzana na masharti yanayowekwa na sheria ya Bunge. Kwa mantiki hiyo, sheria ndogo zote zenye masharti yanayokinzana na masharti yaliyowekwa na sheria za Bunge, zinakuwa ni batili kwa kiwango

zinavyokinzana na sheria mama kama inavyoelekezwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

2.4.3 Dosari ya kuweka Masharti yasiyo na Uhalisia

Mheshimiwa Spika, Pamoja na masuala mengine, uandishi wa sheria hulenga kuweka masharti mbalimbali ambayo zao la utekelezaji wake ni kushughulikia, kufanikisha au kutatua jambo fulani miongoni mwa wanaolengwa na masharti yanayohusika.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya uchambuzi wa Kamati yanabainisha masharti yaliyowekwa na sheria ndogo ambayo utekelezaji wake hauna uhalisia ikilinganishwa na lengo la sheria ndogo. Dosari hiyo imebainika katika **Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, 2024 (TS Na. 30 la 12 Januari, 2024).**

Mheshimiwa Spika, dosari ya kukosa uhalisia ilibainika katika **Kifungu cha 7** kinachohusu udhibiti wa kelele kwa shughuli mbalimbali za kijamii. Kamati ilibaini Kifungu kimeweka sharti kwa mtu yeyote anayetaka kutumia kangavuke kupata kibali cha Halmashauri pasipo kuonesha muda wa kibali hicho kutumika kama ni kwa siku, wiki, mwezi, mwaka au kipindi cha muda wa kutumia Kangavuke na mazingira yanayosababisha kuomba kutumia kangavuke.

Uwekaji masharti hayo unaleta mkanganyiko miongoni mwa wasimamizi na walengwa wa kifungu hicho na hivyo kutokidhi dhima ya kufafanua utekelezaji wa sheria mama na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha dosari nyingine ya kukosa uhalisia inatokana na kifungu kuweka sharti la kupata kibali cha

Halmashauri kwa kitu kingine chochote pasipo kubainisha kitu kinachohusika. Masharti hayo yamewekwa bila kuwa na mipaka ya mambo hayo, jambo linaloweza kugusa upana mkubwa usiokusudiwa na sheria ndogo hii au kutoka nje ya wigo wa mambo yaliyokusudiwa au kutafsiriwa hadi kwenye mambo mengine yanayowekewa utaratibu na sheria nyingine ikasababisha ukinzani au mkanganyiko.

2.4.4 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya misingi ya uandishi wa sheria ni kuwezesha sheria za nchi kufanikisha hatua za serikali kisera na kisheria ili kueleweka kwa urahisi miongoni mwa watu au wananchi wanaoguswa pamoja na wanaosimamia au wenye jukumu la kuzitafsiri. Bunge linapotunga sheria huzingatia misingi ya uandishi ambayo huwezesha mawazo ghafi kuwekwa katika ukamilifu unaoeleweka na wenye maana halisi kiutekelezaji. Kazi nzuri ya Mwandishi Mkuu wa Sheria Nchini inaliwezesha Bunge kuzingatia misingi ya uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Spika, iwapo Bunge ambalo ndilo lenye mamlaka kamili ya utungaji wa sheria huzingatia misingi ya uandishi, sheria ndogo zinatokana na sheria za Bunge nazo zinapaswa kuandikwa kwa kuzingatia misingi thabiti ya uandishi wa sheria. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha kwamba, zipo sheria ndogo zenye dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria. Athari za dosari hiyo, ni sheria ndogo kutokueleweka vizuri na kukosa uhakika wa masharti yake kioutekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa Sheria Ndogo zenye dosari hiyo ni ***Regulations under The Atomic Energy (Protection from Ionizing***

and Non-Ionizing Radiation), 2023 (*TS* ***Na. 840/ 17 Novemba, 2023)***. Tatizo la uandishi lilibainika katika Kanuni ya 8(1), ambayo inaweka masharti kwamba, mtu yeyote anayekusudia kufanya jambo lililotajwa bayana katika Kanuni hizi, atalazimika kuitaarifu Tume kwa namna ilivyoelekezwa na Tume. Isivyo bahati, Kanuni hazina maelezo yanayoweka utaratibu unaostahili kufuatwa katika kutekeleza masharti ya kuitaarifu Tume kuhusu kusudio la kufanya jambo lililobainishwa kwenye kanuni hizi. Kwa matiki hiyo dosari hiyo ya kiuandishi inasababisha kasoro ya ukamilifu wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, ikiwa Bunge lako tukufu litafumbia macho dosari za uandishi zinazobainika kuwepo katika sheria ndogo, upo uwezekano wa dosari hizo kukwamisha utekelezaji mzuri wa sheria zinazotungwa na Bunge. Hivyo, Bunge halipaswi kuruhusu madaraka yake ya kuweka kanuni yatumike kuwezesha sheria ndogo zisozozingatia misingi thabiti ya uandishi wa sheria.

2.4.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida majedwali katika sheria yoyote hulenga kutoa ufafanuzi zaidi na kutimiza malengo ya kifungu cha sheria kinachohusika. Kwa minajili hiyo, Jedwali sheria likiwa na dosari kwenye uandishi wake, linaweza kukwamisha ufafanuzi uliokusudiwa na hatimaye kukwamisha lengo la sheria inayohusika. Matokeo ya uchambuzi yanabainisha sheria ndogo zenye dosari ya uandishi wa majedwali.

Mheshimiwa Spika, dosari hizo ni pamoja na kutorejea vifungu sahihi vinavyoyaanzisha na jedwali, kutokamilika katika maudhui

ya Jedwali au Jedwali kuwa na maudhui yanayokanganya. Mfano wa sheria ndogo zenye dosari za uandishi wa majedwali ni **Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 (TS Na. 39/19 Januari, 2024)**.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Kwanza linalohusu utozaji wa ada au ushuru kwa ajili ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri limebainika kuandikwa kwa namna inayoacha utata. Sehemu ya Kwanza ya Jedwali hilo inaweka ada ya vibali vya burudani ya kandanda kwa viwango vya shilingi 1,000/= kwa mtu mzima, na shilingi 500/= kwa mtoto, pasipo kuonesha namna ya utozaji wake. Uandishi huo unaacha utata kuhusu burudani inayohusika kwenye ada inayotajwa. Ufafanuzi hauoneshi iwapo ada ya vibali ni kwa burudani ya viwanjani au kwa vibanda vya kuonesha kandanda. Hali hii inaweza kuleta utata na kutokueleweka kwa sheria ndogo hizi.

Mheshimiwa Spika, dosari ya kutoainishwa kwa namna ya utozaji wa ushuru inaweza kuwa ni chanzo cha utozaji holela na kwa kuzingatia utashi, hivyo kuathiri malengo ya ukusanyaji wa ushuru yaliyokusudiwa na sheria ndogo. Jambo hilo haliendani na nia ya Bunge. Kamwe Bunge haliwezi kukasimu madaraka yake kwa lengo la kuweka utata katika sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, kipimo kikuu kilichotumika ambacho kinagusa masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, kimesaidia kubaini jumla ya sheria ndogo thelathini na nane (38) zenye dosari za namna kuu **nne** kama ilivyobainishwa kwenye **Kiambatisho Na. 01**. Mifano ya sheria ndogo hizo imetajwa ambapo sheria ndogo tano zimejitokeza kwenye mifano hiyo. Jambo muhimu

kwa Bunge ni kuazimia kufanyika kwa marekebisho ili kuepuka madhara ya dosari hizo katika mfumo wa sheria na kwa maisha ya wananchi wanaowakilishwa Bungeni.

2.5 Majumuisho ya Sehemu ya Pili

Mheshimiwa Spika, maelezo yote katika sehemu ya pili yanajengwa katika msingi wa masharti ya Katiba, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na Kanuni za Bunge. Misingi hiyo imetaka uchambuzi wa sheria ndogo ufanyike kwa kuwa mamlaka ya kuweka sheria za nchi ni Bunge, na kwamba, wananchi wanaowakilishwa Bungeni wanastahili kuwa na ustawi unaowekewa masharti na sheria. Kwa maelezo hayo ruhusa ya Bunge kukasimu madaraka haina maana kwamba Bunge linaruhusiwa kung'atuka katika madaraka ya kuweka sheria za nchi. Hivyo, Bunge linawajibika kufuatilia sheria zilizotungwa kutokana na madaraka ya Bunge kukasimiwa kwenye mamlaka nyingine. Kutokufuatia au kutojishughulisha na namna sheria ndogo zilizotungwa zinawaathiri wananchi, ni kutelekeza madaraka ya kutunga sheria. Bunge hili haliwezi kufanya kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa mamlaka ya utendaji kuzingatia maazimio ya Bunge hususan maazimio kuhusu dosari za sheria ndogo. Dosari katika heria ndogo zisiporekebishwa, athari yake itaendelea kuwa mbaya kwenye dhima ya sheria za nchi na kwamba zitakwamisha azma ya Serikali na Lengo la Bunge. Aidha, hatua za utekelezaji wa maazimio ya Bunge zisizotimia zimeoneshwa na kwa kweli si hali inayofaa.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika sehemu ya kwanza na sehemu ya Pili, Bunge ndicho chombo chenye mamlaka kamili ya kuiweka sheria ndogo na kwamba lina dhima kwa sheria za nchi. Uzuri au ubaya wa sheria za nchi ni dhima ya Bunge. Ziwe ni sheria mama, sheria nyingine za Bunge au sheria ndogo, dosari zake zisiporekebishwa, Bunge linaendelea kuwa na dhima kwa uzuri au ubaya wake. Kwa msingi huo, Kamati ina maoni na mapendekezo kutokana na matokeo ya Uchambuzi yanayobainishwa kwenye **Kiambatisho Na. 01** na **Kiambatisho Na. 02.** Maoni na mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo -

3.2 Maoni

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa sheria ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya wananchi katika utekelezaji wake, ninaliomba Bunge lako lipokee mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii na kuyafanyia kazi. Kwa madhumuni hayo, naomba kudhihirisha mtazamo wa Kamati unaotokana na uchambuzi kama ifuatavyo: -

(i) Dosari ya Sheria Ndogo kukinzana na masharti ya Katiba inaathiri uthabiti wa mfumo wa sheria za nchi. Hivyo, kuwa na madhara wakati wa utekelezaji, kama vile ukiukaji wa haki za kimsingi na uhuru unaohakikishwa na katiba, matumizi mabaya ya mamlaka, ukiukwaji wa uhuru wa raia na kudhoofika kwa utawala wa sheria.

(ii) Dosari ya sheria ndogo kuwa na masharti yanayokinzana na Sheria Mama au na Sheria nyingine za nchi inaweza kukwamisha azma ya sheria mama au sheria nyingine za Bunge. Hivyo, kuvuruga mfumo wa sheria za nchi, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa na Bunge.

(iii) Sheria ndogo kuwa na masharti yasiyo na uhalisia inasababisha mkanganyiko katika utekelezaji wa masharti hayo. Hali hiyo inaweza kuwa ni chanzo cha kukwamisha malengo ya sheria mama pia uwezekano wa mazalia ya kero kwa Wananchi.

(iv) Dosari ya sheria ndogo kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria inaathiri ubora wa sheria kwenye ufasaha, usahihi, ukamilifu na kueleweka. Hivyo, kuwa na madhara wakati wa utekelezaji, jambo ambalo halikuwa lengo la Bunge wakati wa kukasimu madaraka yake.

(v) Dosari za uandishi wa majedwali katika sheria inaweza kusababisha sheria iliyoandikwa isieleweke ipasavyo kutokana na kukosekana kwa ufafanuzi uliokusudiwa kwenye Jedwali. Hivyo, kukwamisha utekelezaji wa baadhi ya masharti ya sheria ndogo na sheria mama.

(vi) Kutokamilisha utekelezaji kwa maazimio ya Bunge kuhusu marekebisho ya sheria ndogo kunachelewesha utatuzi wa kero za wananchi. Hivyo, Bunge ambalo ni mamlaka kuu ya utungaji wa sheria, halipaswi kuruhusu ucheleweshaji huo.

3.3 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, kwa msingi wa maoni ya Kamati yanayotokana na shughuli za **uchambuzi wa sheria ndogo** na **uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**, Kamati inapendekeza mambo

saba (07) kwa mfumo wa hoja Bungeni kama inavyoelekeza Kanuni ya 61 ya Kanuni za Bunge. Mambo hayo saba na mapendekezo yanayoyahusu ni kama ifuatavyo: -

3.3.1 Sheria Ndogo kuwa na Masharti yanayokinzana na Masharti ya Katiba

KWA KUWA, dosari ya Sheria Ndogo ya kukinzana na masharti ya Katiba, kama ilivyobainika kwenye sheria ndogo zilizochambuliwa ikiwemo **Sheria Ndogo ya (Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 (TS Na. 38/19 la Januari, 2024)**, ni ukiukwaji wa masharti ya Ibara ya 64 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

NA KWA KUWA, Ibara ya 64 (5) ya Katiba inakataza sheria yoyote zikiwemo sheria ndogo inayobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga sheria ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 01** cha Taarifa hii, zirekebishe dosari za sheria ndogo zinazohusika.

3.3.2 Dosari ya kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi

KWA KUWA, dosari ya sheria ndogo kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, mfano **Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 (TS Na. 920 22 Disemba, 2023)**, inaweza:

(i) kukwamisha azma ya sheria mama au sheria nyingine za Bunge;

(ii) kuvuruga mfumo wa sheria za nchi, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa na Bunge; na

NA KWA KUWA, matokeo ya dosari hizo yanakwamisha azma ya Bunge kutunga sheria mama na kukasimu sehemu ya madaraka yake kwa mamlaka nyingine serikalini ili ifanye ufafanuzi wa sheria mama kwa namna inayotekelezeka kwa urahisi na kiufundi,

KWA HIYO BASI, **Bunge linaazimia kwamba**, Mamlaka zilizotunga sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi kama ilivyobainishwa katika **Kiambatisho Na. 01** cha Taarifa hii, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hiyo.

3.3.3 Dosari ya Kuweka Masharti yasiyo na Uhalisia

KWA KUWA, dosari ya sheria ndogo kuwa na masharti yasiyo na uhalisia kama ilivyoonekana katika sheria ndogo zilizochambuliwa ikiwemo **Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, 2024 (TS Na. 30 la 12 Januari, 2024).**

NA KWA KUWA, dosari hiyo inaweza:

(i) kukwamisha utekelezaji wa sheria ndogo yenyewe;

(ii) kukwamisha utekelezaji wa masharti ya sheria mama; na

(iii) kuwa chanzo cha kero miongoni mwa wananchi.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na

dosari ya kuweka masharti yasiyo na uhalisia kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 01**, zirekebishe dosari hiyo ili kufikia malengo yoliyokusudiwa.

3.3.4 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria

KWA KUWA, dosari ya sheria ndogo kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria, kama ilivyobainika kwenye sheria ndogo zilizochambuliwa ikiwemo ***Regulations under The Atomic Energy (Protection from Ionizing and Non-Ionizing Radiation), 2023*** **(TS Na. 840/ 17 Novemba, 2023),** inaathiri ubora wa sheria kwenye ufasaha, usahihi, ukamilifu na kueleweka kwake,

NA KWA KUWA, athari hizo mbaya kwenye sheria:

(i) zinaathiri azma ya Bunge kufanikisha utekelezaji wa hatua za serikali kisera kupitia sheria za Bunge na sheria ndogo;

(ii) zinakwamisha nia ya Bunge kuwezesha sheria kueleweka kwa urahisi miongoni mwa watekelezaji wa sheria au wanaoguswa na masharti ya sheria inayohusika; na

(iii) zinaonesha ukiukaji wa misingi isiyopaswa kukiukwa na Bunge lenyewe ambalo ndilo mamlaka kuu ya utungaji wa sheria,

KWA HIYO BASI, **Bunge linaazimia kwamba,** Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 01**, zirekebishe dosari hiyo ili kuleta tija iliyokusudiwa.

3.3.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali

KWA KUWA, dosari za uandishi wa majedwali katika sheria ndogo kama ilivyobainika kwenye uchambuzi unaoripotiwa na kuoneshwa kwenye Jedwali Na. 01 la Taarifa hii ikiwemo **Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 (TS Na. 39/19 Januari, 2024),** inaweza kukwamisha kueleweka kwa sheria,

NA KWA KUWA, mkwamo huo unaotokana na dosari za uandishi wa majedwali unaweza kusababisha -

(i) changamoto katika utekelezaji wa sheria ndogo inayohusika, jambo ambalo halikuwa lengo la Bunge kukasimu madaraka ya kutunga sheria kwa mamlaka zinazohusika; na

(ii) kufifia kwa madhumuni ya Bunge kutunga sheria inayotekelezwa ikitegemea ufafanuzi unaopaswa kutolewa na sheria ndogo,

KWA HIYO BASI, **Bunge linaazimia kwamba,** Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zilibainika kuwa na majedwali yenye dosari za kiuandishi kama inavyobainishwa kwenye **Kiambatisho Na. 01**, zifanye marekebisho ili kuepusha madhara ya dosari zilizobainika.

3.3.6 Kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio kuhusu Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na Dosari

KWA KUWA, Dosari zote zilizobainika katika uchambuzi kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Uchambuzi, ambalo ni **Kiambatisho Na. 01** zinahitaji kurekebishwa inavyostahili,

NA KWA KUWA, kutokurekebishwa kwa dosari zilizobainika kutokana na uchambuzi ni jambo ambalo -

(i) linakiuka misingi ya sheria za nchi na kuathiri tija na ufanisi katika utekelezaji;

(ii) litaendeleza madhara ya dosari hizo katika mfumo wa sheria za nchi; na

(iii) halistahili kuachwa na Bunge liendelee kuwepo kwa kuwa mamlaka yenye dhima na uzuri au ubaya wa sheria za nchi ni Bunge,

KWA HIYO BASI, **Bunge linaazimia kwamba**, Mamlaka zote zinazohusika na sheria ndogo zenye dosari kama zilivyotajwa katika **Kiambatisho Na. 01** cha Taarifa hii, ziwasilishe Taarifa ya utekelezaji wa maazimio yote kuhusu dosari za sheria ndogo kwa Katibu wa Bunge ifikapo saa tisa na nusu ya tarehe 20 Disemba, 2024.

3.3.7 Kutokamilika kwa Utekelezaji wa Maazimio ya Kurekebisha Sheria Ndogo

KWA KUWA, Maazimio ya Bunge yaliyohusu kurekebisha dosari ishirini na tisa (29) katika sheria ndogo, yalilenga kuondoa madhara ya dosari hizo, ikiwemo uwezekano wa kusababisha kero kwa wananchi;

NA KWA KUWA, kutokamilisha maazimio ya Bunge yanayolenga kuondoa dosari za sheria ndogo ni jambo ambalo -

(i) linalochelewesha utatuzi wa kero za wananchi wanaolitegemea Bunge kusimamia maslahi yao.

(ii) Halizingatii dhima ya Bunge katika sheria za nchi likihusika kwa sheria mbaya au nzuri nchini,

KWA HIYO BASI, **Bunge linaazimia kwamba**, Mamlaka ambazo hazijakamilisha utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, zikamilishe mchakato wa marekebisho na kwamba, ifikapo saa tisa na nusu ya tarehe 27 Septemba, 2024 ziwe zimewasilisha kwa Katibu wa Bunge, taarifa za utekelezaji wake zenye ushahidi wa kurekebishwa kwa dosari zilizobainika katika sheria ndogo zinazohusika.

3.4 Majumuisho ya Sehemu ya Tatu

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya tatu, taarifa hii imebainisha mambo saba yaliyowekewa mtazamo wa jumla na Kamati. Mtazamo huo unatokana na misingi iliyobainishwa katika sehemu ya pili ya Taarifa hii ambayo inahusu nafasi ya Bunge katika sheria za nchi, uhusiano wa Bunge na Wananchi, lengo kuu la Serikali kwa mujibu wa Katiba na matarajio ya Wananchi. Misingi hiyo imewekwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii pia imebainisha mapendekezo **saba** yanayotokana na mtazamo wa Kamati kuhusu mambo makuu saba yaliyobainishwa. Bunge linashauriwa kuyapokea mapendekezo hayo ili yawe maazimio ya Bunge kwa msingi wa masharti ya Katiba, Kanuni za Bunge na Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 ya Sheria za Tanzania.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika vikao vya Bunge. Kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano Kumi na Tano pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa kipekee wa Wajumbe wa Kamati hii katika usomaji na kufanya rejea nyingi kwa pamoja na umakini wao kwenye maandishi bila kuchoka ni mambo yaliyofanikisha taarifa hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, (Mb) – Mwenyekiti;
2. Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan, (Mb) M/ Mwenyekiti;
3. Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb Mjumbe;
4. Mhe. Amour Khamis Mbarouk, (Mb) Mjumbe;
5. Mhe. Jacob Tarimo Priscus, (Mb) Mjumbe;
6. Mhe. Khamis Ali Vuai, (Mb) Mjumbe;
7. Mhe.Eng.Dkt.Leonard M. Chamuriho,(Mb) Mjumbe;
8. Mhe. Simai Hassan Sadiki, (Mb) Mjumbe;
9. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, (Mb) Mjumbe;
10. Mhe. Aloyce Andrew Kwezi, (Mb) Mjumbe;
11. Mhe. Hamida Mohammed Abdallah, (Mb) Mjumbe;
12. Mhe. Ally Mohamed Kassinge, (Mb) Mjumbe;

13. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, (Mb) Mjumbe;
14. Mhe. Maryam Omar Said, (Mb) Mjumbe;
15. Mhe. Zulfa Mmaka Omar, (Mb) Mjumbe;
16. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, (Mb) Mjumbe;
17. Mhe. Amina Bakar Yusuf, (Mb) Mjumbe;
18. Mhe. Latifa Khamis Juakali, (Mb) Mjumbe;
19. Mhe. Benaya Lyuka Kapinga, (Mb) Mjumbe;
20. Mhe. Nape Moses Nnauye, (Mb) Mjumbe; na
21. Mhe. Ummy Ally Mwalimu, Mb Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, Kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mhe. William Vanging'embe Lukuvi, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa uratibu wake uliowezesha Kamati kupata taarifa na majibu ya Serikali. Niwashukuru pia Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao katika vikao vya uchambuzi wa sheria ndogo na vikao vya kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Vilevile, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa huduma bora za kiutawala na uratibu wanazoipatia Kamati na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, Sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa hii ili yawe Maazimio ya Bunge katika Mkutano wake wa Kumi na Sita wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.



Jasson Samson Rweikiza, Mb
MWENYEKITI
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo
4 Septemba, 2024

KIAMBATISHO NA. 1

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO

JEDWALI LA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KATIKA MKUTANO WA KUMI NA NNE NA MKUTANO WA KUMI NA TANO

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KWENYE MKUTANO WA KUMI NA NNE						
1.	**TS Na. 1** 5 Januari, 2024	*Rules under the Accountants and Auditors (Appeals Board), 2024* **(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 25(3))**	*The Accountants and Auditors (Registration) Act, (Cap. 286)*	Wizara ya Fedha	1. **Kanuni ya 3** imetoa tafsiri ya maneno mbalimbali ikiwemo neno "Respondent". **<u>Tatizo</u>** Kanuni haijaweka tafsiri ya tafsiri ya maneno "appellant" na "applicant". Kutokuwekwa kwa tafsiri hiyo kunasababisha kukosekana kwa ufafanuzi kuhusu maneno hayo na namna ambavyo yatatumika katika Kanuni hizi. 2. **Kanuni ya 6** inaweka fursa kwa mhusika yoyote katika shauri, kuomba uamuzi	1. Kanuni ifabyiwe marekebisho kwa kuongeza tafsiri ya maneno "appellant" na "applicant" 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la kuomba uamuzi

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					utafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili. **<u>Tatizo</u>** Kanuni inakikuka matakwa ya Kifungu cha 84A cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinachoweka ulazima kwa uamuzi kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. (Sheria nyingine)	ulioandikwa kwa lugha ya kiingereza kutafsiriwa kwa lugha ya kiswahili.
					3. **Kanuni ya 9** inampa uwezo Msajili kurejesha nyaraka zozote zitakazobainika kuwa na makosa mbalimbali ili zifanyiwe marekebisho. **<u>Tatizo</u>** Kanuni haijaweka muda unaopaswa	3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili muda wa siku kumi na nne ili kufanya marekebisho ya nyaraka zilizorejeshwa.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					kuzingatiwa na mhusika katika kufanya marekebisho yanayohusika. Kukosekana kwa muda mahsusi kunaweza kusababisha kukosekana muongozo kuhusu muda unaostahili. 4. **Kanuni ya 35** inaweka utaratibu wa kusikiliza maombi ya rufaa ya mrufani iwapo mjibu rufaa hakufika mbele ya Bodi siku iliyopangwa kwa ajili ya kusikiliza rufaa. **<u>Tatizo</u>** Kanuni inaeleza kuwa, Bodi itaendelea na shauri,	4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kuwa Bodi itaendelea kusikiliza shauri upande mmoja (*Ex-parte*).

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					pasipo kuonesha kuendelea na shauri kunakokusidiwa ni usikilizaji wa shauri la upande mmoja au ni kuendelea kwa namna nyingine. Aidha Kanuni haioneshi utaratibu utakaofuatwa katika kuendelea huko. Hali hiyo inayoweka utata wa masharti ya Kanuni ya 35 inasababisha kutokutabirika kwa hatua utaratibu unaoweza kufuatwa iwapo mjibu rufaa hajafika. 5. **Fomu A** katika **Jedwali la Kwanza** inahusu notisi ya kusudio la kukata rufaa.	5. Fomu A ifanyiwe marekebisho ili kurejea Kanuni ya 7(2)(e)

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Fomu ina makosa ya uandishi kwa kurejea kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 8(2)(e)** ambayo si sahihi (sahihi ni **Kanuni ya 7(2)(e))**. Kosa hilo linasababisha mkanganyiko kutokana na kutoendana na misingi ya uandishi wa Fomu kwenye Majedwali na hivyo kutatiza ufafanuzi wa masharti ya jumla ya Kanuni hizi. 6. **Fomu B** katika Jedwali la Kwanza inahusu Notisi ya Anuani ya Huduma *(Notice of Address for Service)*	6. **Fomu B** ifanyiwe marekebisho ili kurejea Kanuni ya 7(5)(c)

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Fomu ina makosa ya uandishi kwa kurejea kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 8(5)(c)** ambayo si sahihi (sahihi ni **Kanuni ya 7(5)(c))**. Kosa hilo linasababisha mkanganyiko kutokana na kutoendana na misingi ya uandishi wa Fomu kwenye Majedwali na hivyo kutatiza ufafanuzi. 7. **Fomu C** katika Jedwali la Kwanza inahusu uthibitisho wa kusambaza na kuwasilisha nyaraka	7. **Fomu C** ifanyiwe marekebisho ili kurejea Kanuni ya 12(2).

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Fomu ina makosa ya uandishi kwa kurejea kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 13(2)** ambayo si sahihi (sahihi ni **Kanuni ya 12(2)**). Kosa hilo linasababisha mkanganyiko kutokana na kutoendana na misingi ya uandishi wa Fomu kwenye Majedwali na hivyo kutatiza ufafanuzi 8. **Fomu D** katika Jedwali la Kwanza inahusu Hati ya Rufaa **<u>Tatizo</u>** Fomu ina makosa ya uandishi kwa kurejea kuanzishwa chini ya	8. **Fomu D** ifanyiwe marekebisho ili kurejea Kanuni ya 8(4)

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					Kanuni ya 9(4) ambayo si sahihi (sahihi ni **Kanuni ya 8(4)**). Kosa hilo linasababisha mkanganyiko kutokana na kutoendana na misingi ya uandishi wa Fomu kwenye Majedwali na hivyo kutatiza ufafanuzi (Jedwali) 9. **Fomu E** katika Jedwali la Kwanza inahusu Majibu ya Hati ya Rufaa **<u>Tatizo</u>** Fomu ina makosa ya uandishi kwa kurejea kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 16(3)** ambayo si sahihi	9. **Fomu E** ifanyiwe marekebisho ili kurejea Kanuni ya 14(3)

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					(sahihi ni **Kanuni ya 14(3)**). Kosa hilo linasababisha mkanganyiko kutokana na kutoendana na misingi ya uandishi wa Fomu kwenye Majedwali na hivyo kutatiza ufafanuzi. 10. **Fomu E** katika Jedwali la Kwanza inahusu Majibu ya Hati ya Rufaa na Taatira ya kuingilia (*Statement of Intervention)*. **<u>Tatizo</u>** Kuna **Fomu E** mbili zenye zenye maudhui tofauti **Fomu E** ya Kwanza ni kuhusu Majibu ya Hati	10. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka sawa mtiririko sahihi wa herufi katika Fomu

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					ya Rufaa na **Fomu E** ya pili ni kuhusu Taarifa ya kuingilia (*Statement of Intervention)*. Makosa ya uandishi katika Majedwali zinaleta mkanganyiko wa usomaji wa mzuri wa Kanuni, pia changamoto wakati wa kufanya rejea ya Fomu inayohusika.	
2.	**TS Na. 2** 5 Januari, 2024	*Regulations under the Civil Aviation (Heliports), 2024* **(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 4)**	*The Civil Aviation Act, (Cap. 80)*	Wizara ya Uchukuzi	**Kanuni ya (98)** pamoja na masuala mengine inaipa uwezo Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania kusitisha kwa muda (*suspension*) leseni, cheti, idhini au hati nyingine zilizotolewa chini ya Kanuni hizi.	Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sababu zitakazosababisha kuondolewa zuio la muda (Suspension).

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Kanuni haioneshi mazingira yanayoweza kuondolea kwa zuio la muda la leseni iliyotolewa. Hali hiyo inaweza kutatiza uzingatiaji wa misingi ya haki kuhusu leseni, cheti, idhini au hati nyingine zilizotolewa na Mamlaka kwa wahusika iwapo watarekebisha kasoro au dosari zilizosababisha zuio.	
3.	**TS Na. 3** 5 Januari, 2024	*Regulations under the Civil Aviation (Operation of Aircraft - Helicopter Operations), 2024* **(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 4)**	*The Civil Aviation Act, (Cap. 80)*	Wizara ya Uchukuzi	**Kanuni ya 132** inatoa fursa kwa mtu kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania kuhusu ukiukwaji wa masharti ya sheria, kanuni na amri.	Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha utaratibu utakaotumika kuwasilisha taarifa za ukiukwaji.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Kanuni haioneshi utaratibu wa namna ya kufikisha taarifa za ukiukwaji zinazohusika kwa Mamlaka. Kutokubainishwa kwa namna ya kuwasilisha taarifa ni jambo linalotatiza kutimia kwa lengo la sheria ndogo hizi kutokana na kukanganya wakati wa utekelezaji.	
4.	**TS Na. 5** 5 Januari, 2024	*Regulations under the Civil Aviation (Certification, Licensing and Registration of Aerodromes), 2024* **(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 4)**	*The Civil Aviation Act, (Cap. 80)*	Wizara ya Uchukuzi	1. **Kanuni ya 7** inaonesha masharti ya kuzingatia ili kupata cheti cha kuendesha *aerodrome*. **<u>Tatizo</u>** **Kanuni ya 7(2)(i)** inaipa uwezo Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kuwa, nyaraka zitakazoombwa ni zile zinazohusiana na masharti ya Kanuni ya 7.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					wa kuomba nyaraka nyingine zaidi ya zilizotajwa, pasipo kuonesha kuwa nyaraka hizo za ziada ziwe zinazohusu vigezo vya kutambulisha viwango vya kuendesha *aerodrome*. Hali hii inafifisha lengo la Kanuni kutoa ufafanuzi wa masharti ya sheria mama.	
					2. **Kanuni ya 17(2)(k)** inahusu viambatisho vinayopaswa kuambatishwa katika maombi ya leseni ya kuendesha *aerodrome*.	2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kuwa, nyaraka zitakazoombwa ni zile zinazohusiana na masharti ya Kanuni ya 7(2)(k).

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> **Kanuni ya 17 (2)(k)** inalipa Mamlaka nguvu ya kutaka nyaraka nyingine yoyote bila kutaja nyaraka hizo. Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa. 3. **Kanuni ya 28(2)(k)** inahusu viambatisho vinavyopaswa kuambatishwa katika maombi ya usajili wa kuendesha *aerodrome*. **<u>Tatizo</u>** **Kanuni ya 28 (2)(k)** inalipa Mamlaka nguvu ya kutaka nyaraka nyingine	3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kuwa, nyaraka zitakazoombwa ni zile zinazohusiana na masharti ya Kanuni ya 28(2)(k)

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					yoyote bila kutaja nyaraka hizo. Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa. 4. **Kanuni ya 43** inamtaka mwendesha *aerodrome* kuhakikisha kuwa anakuwa na idadi nzuri ya watumishi wenye vigezo na ujuzi wa kuendesha na kufanya marekebisho ya *aerodrome*. **<u>Tatizo</u>** Kanuni imeeleza kwa jumla kuhusu idadi, vigezo na ujuzi pasipo kufafanua idadi inayokusudiwa,	4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kurejea Muongozo TCAA/QSP/SR/AC/AGA-024 Advisory Circular on Competence of Personnel at Certified Aerodrome

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					vigezo vya watumishi hao na aina ya ujuzi wanaopaswa kuwa nao. Kutofafanuliwa kwa mambo hayo ni kutofanikisha lengo la sheria ndogo kufafanua masharti ya sheria mama, hivyo kuna uwezekano wa kukwamisha ufafanuzi wa sheria mama.	
					5. **Kanuni ya 64** pamoja na masuala mengine inaipa uwezo Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania kusitisha kwa muda au kufuta leseni, cheti, idhini au hati nyingine iliyotolewa chini ya Kanuni hizi.	5. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sababu zitakazosababisha kuondolewa zuio la muda (Suspension).

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Kanuni haioneshi mazingira yanayoweza kusababisha kuondolewa kwa zuio la muda la leseni iliyotolewa. Hali hiyo inaweza kutatiza uzingatiaji wa misingi ya haki kwa wahusika waliosahihisha kasoro au dosari zilizosababisha kusitishwa kwa leseni zao kwa muda.	
					6. **Kanuni ya 64(3)** inamtaka mhusika aliyepewa notisi ya kusitishiwa cheti, leseni au usajili wake kwa muda, kuwasilisha utetezi wake kwa Mamlaka	6. Kanuni ifanyiwe ifanyiwe marekebisho kwa kurejea Kanuni sahihi.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					ndani ya muda usiozidi siku kumi na nne. **<u>Tatizo</u>** Kanuni imefanya rejea ya **Kanuni ndogo ya (2)** ambayo haipo katika Kanuni hizi. 7. **Kanuni ya 70(1)** inazungumzia kuhusu maombi ya mapitio ya msamaha wa usahihi na utii wa masharti yaliyowekwa na sheria ndogo hizi. **<u>Tatizo</u>** Kanuni hazioneshi muda utakaotumiwa na Mamlaka kushughulikia maombi ya mapitio.	7. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kurejea Muongozo TCAA - O- GEN015A Procedure for Review and Processing of Exemption.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					Kutokuwekwa kwa muda mahsusi kunaweza kusabisha ucheleweshaji wa mapitio hivyo kukwamisha shughuli za wanaohusika. 8. **Kanuni ya 80(3) (3)** inaipa uwezo Mamlaka kutoza asilimia 40 ya uthibitisho wa ada inayotumika ya tathmini ya minara ya angani *(evaluation of aerial mast)*. **<u>Tatizo</u>** Kanuni haioneshi chanzo ambacho asilimia 40 itatozwa na Mamlaka.	8. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha msingi wa tozo ya asilimia 40.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					9. **Kanuni ya 82(6)(a)** inaweka tafsiri ya maneno "*en-route obstacle*". **<u>Tatizo</u>** Kanuni ina makosa ya uandishi kwa kurudia maudhui ya aya (a) katika aya (b).	9. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta maudhui yanayojirudia.
					10. **Kanuni ya 95(1)** inahusu utafiti wa anga na tathmini ya hatari (*Aeronautical study and risk assessment*) **<u>Tatizo</u>** Kanuni ina makosa ya uandishi kwa kukosa ukamilifu wa sentensi mara baada ya neno la mwisho la sentensi "*Where an*	10. Kanuni ifanyiwe marekebisho kuondoa makosa ya uandishi ili kuleta maana iliyokusudiwa.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					aerodrome does not meet the requirements of the prescribed standards, the Authority may determine, after carrying out" Kukosekana kwa ukamilifu kunasababisha kutokueleweka kwa kanuni na hivyo kutokidhi lengo lililokusudiwa.	
5.	**TS Na. 6** 5 Januari, 2024	*Regulations under the Civil Aviation (Instruments and Equipment), 2024* **(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 4)**	*The Civil Aviation Act, (Cap. 80)*	Wizara ya Uchukuzi	**Kanuni ya 190** pamoja na masuala mengine inaipa uwezo Mamlaka wa kusitisha kwa muda au kufuta leseni, cheti, idhini au hati nyingine iliyotolewa chini ya Kanuni hizi.	Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sababu zitakazosababisha kuondolewa zuio la muda (Suspension).

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Kanuni haioneshi mazingira yanayoweza kuondolewa kwa zuio la muda la leseni iliyotolewa. Hali hiyo inaweza kutatiza uzingatiaji wa misingi ya haki kuhusu leseni, cheti, idhini au hati nyingine zilizotolewa na Mamlaka kwa wahusika iwapo watarekebisha kasoro au dosari zilizosababisha zuio.	
6.	**TS Na. 7** 5 Januari, 2024	*Regulations under the Civil Aviation (Aerodrome Design and Operations), 2024* **(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 4)**	*The Civil Aviation Act, (Cap. 80)*	Wizara ya Uchukuzi	1. **Kanuni ya 4(5)** inaelekeza matumizi ya kipimo cha *International System of Units* (ambacho kinatumia vipimo vya kama vile mita, kilometa na sentimita).	1. Kanuni ya ifanyiwe marekebisho ili kutambua aina nyingine za vipimo zaidi ya SIU

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Tafsiri ya neno *vicinity* chini ya **Kanuni ya 3** imetumia kipimo cha futi ambacho kinatofautiana na *International System of Units* iliyoelekezwa na Kanuni ya 4(5) ambayo haina kipimo cha futi. 2. **Kanuni ya 11** inahusu *Aerodrome reference code* **<u>Tatizo</u>** Maudhui ya Kanuni ndogo ya (6) na (7) hayahusiani na maudhui ya Kanuni ya 11 kuhusu *Aerodrome reference code*.	2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta maudhui ya kanuni ndogo ya (6) na (7).

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					3. **Kanuni ya 14** inahusu upatikanaji wa taarifa. **<u>Tatizo</u>** Kanuni imetumia neno NOTAM ambalo halijawekewa tafrisi katika Kanuni ya 3 inayoweka tafsiri ya meneno mbalimbali badala yake imewekwa katika Jedwali la Sita. 4. **Kanuni ya 21** inahusu *Aerodrome and runway elevations*. **<u>Tatizo</u>** **Kanuni ndogo ya (1), (2) na (3)** zinatumia kipimo cha futi ambazo ni kinyume na kipimo	3. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuandika kirefu cha neno NOTAM ili kutoa ufafanuzi unakosusidiwa. 4. Kanuni ya ifanyiwe marekebisho ili kutambua aina nyingine za vipimo zaidi ya SIU

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					kilochoelekezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 4(5) ambacho hakihusishi kipimo cha futi. 5. **Kanuni ya 23** inazungumzia kuhusu vipimo vya *Aerodrome* na masuala yanayohusiana na vipimo. **<u>Tatizo la Kwanza</u>** **Kanuni ndogo ya (1)(a), (1)(b) na (1)(f) na (1)(j)** zinatumia kipimo cha futi ambazo ni kinyume na kipimo kilichoelekezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 4(5) ambacho hakihusishi kipimo cha futi.	5. Kanuni ya ifanyiwe marekebisho ili kutambua aina nyingine za vipimo zaidi ya SIU

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo la Pili</u> **Kanuni ndogo ya (1)(h)** imetumia neno VOR ambalo halijatafsiriwa katika Kanuni inayoweka tafsiri za maneno mbalimbali. **<u>Tatizo la Tatu</u>** **Kanuni ndogo ya (5)** imetumia maneno *Area 2* na *Area 3* pasipo wapi yanatoka au ni maeneo gani yanayokusudiwa. 6. **Kanuni ya 25** inahusu vigezo vya uimara wa lami. **<u>Tatizo</u>** Kanuni imeweka tarehe ya kuanza kutumika kwa	6. Kanuni ifanyiwe marekebisho kuweka ndani ya Kanuni tarehe ya kuanza kutumika kwa vigezo vya uimara wa lami

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					masharti katika maelezo ya pembeni "*marginal note*" ya kanuni ambayo hayana nguvu ya kisheria. 7. **Kanuni ya 26** inahusu *Pre-flight altimeter check location.* **<u>Tatizo</u>** **Kanuni ndogo ya (3)** Kanuni ndogo ya zinatumia kipimo cha futi ambacho ni kinyume na kipimo kilochoelekezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 4(5) ambacho hakihusishi kipimo cha futi. 8. **Kanuni ya 27** inazungumzia kuhusu *Declared distances*	7. Kanuni ya ifanyiwe marekebisho ili kutambua aina nyingine za vipimo zaidi ya SIU 8. Kanuni ya ifanyiwe marekebisho ili kutambua aina

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> **Kanuni ndogo ya (1)** Kanuni ndogo ya zinatumia kipimo cha futi ambacho ni kinyume na kipimo kilochoelekezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 4(5) ambacho hakihusishi kipimo cha futi.	nyingine za vipimo zaidi ya SIU
					9. **Kanuni ya 53** inahusu *Width of runway shoulders* **<u>Tatizo</u>** Maudhui ya **Kanuni ndogo ya (2)** yanajirudia kama yalivyo katika aya (1)	9. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta maudhui yanayojirudia.
					10. **Kanuni ya 154** kinahusu alama za maelekezo ya lazima.	10. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta jina la sheria na kifungu wezeshi

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Kanuni ina makosa ya uandishi kwa kurejea jina la sheria mama na kifungu wezeshi katikati **kanuni ndogo ya (4) na (5)**.	katikati ya vifungu vinavyohusika.
					11. **Kanuni ya 299** inaeleza maelezo ya kufuta Kanuni zilizokuwa zinatumika kabla ya kutungwa kwa kanuni hizi. **<u>Tatizo</u>** Kanuni itaja kufutwa kwa *Civil Aviation (Aerodromes) Regulations* na badala yake kutungwa Kanuni za *Civil Aviation (Certification, Licensing and*	11. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kutaja majina sahihi ya Kanuni inayofutwa na Kanuni inayotungwa

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					Registration of Aerodromes) Regulations, 2023. Kanuni zote zinazotajwa hazihusiani na Kanuni hizi.	
					12. **Fomu Na. TCAA/FRM/SR/AGA-07** katika **Jedwali la Kwanza** ihahusu kibali cha ujenzi *wa Aerodrome* inarejea kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 124 na 130**. **<u>Tatizo</u>** **Kanuni ya 124 na 130** zinazorejewa hazihusiani na maudhui yaliyo katika fomu hiyo. Makosa ya urejeaji wa Kanuni zisizo sahihi katika	12. Marekebisho yafanyike kwa kurejea Kanuni sahihi zinazoanzisha **Fomu Na. TCAA/FRM/SR/AGA-07** katika **Jedwali la Kwanza**

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					Majedwali zinaleta mkanganyiko wa usomaji wa mzuri wa Kanuni.	
7.	**TS Na. 8** 5 Januari, 2024	*Regulations under the Civil Aviation (Facilitation of Air Transport), 2024* **(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 4)**	*The Civil Aviation Act, (Cap. 80)*	Wizara ya Uchukuzi	1. **Jedwali la Kwanza** linaonesha mfano wa fomu ya tamko la jumla. **<u>Tatizo</u>** Jedwali lina makosa ya uandishi kwa kurejea kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 3** ambayo maudhui yake hayaendani na Kanuni hiyo. Kwa kufanya hivyo inaharibu mtiririko na kutatiza ufafanuzi uliostahili. 2. **Jedwali la Tatu** linaonesha mfano wa cheti cha uanachama wa	1. **Jedwali la Kwanza** lifanyiwe marekebisho ili krejea Kanuni sahihi inayolianzisha. 2. **Jedwali la Tatu** lifanyiwe marekebisho ili

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					mfanyakazi wa kwenye ndege (*Crew Member Certificates*) **<u>Tatizo</u>** Jedwali linarejea kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 26(2)(a)** ambayo haipo (Kanuni sahihi **26(3)(a)**). Urejeaji huo unasababisha ugumu wa kueleweka kwa masharti ya jumla ya Kanuni hizi.	kurejea Kanuni sahihi inayolianzisha.
8.	**TS Na. 15** 12 Januari, 2024	*Rules under the Land Transport Regulatory Authority (Terms and Conditions for Provision of Regulated Services), 2024*	*The Land Transport Regulatory Authority Act, (Cap. 413)*	Wizara ya Uchukuzi	1. **Kanuni ya 11** inaweka sharti kwa mtoa huduma kuwa na mtumishi mwenye uzoefu wa masuala ya usafirishaji na usimamizi wa shughuli za usafirishaji.	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta sharti llinalomtaka mtoa huduma mwenye vyombo vya usafiri chini ya sita kuwa na mtumishi mwenye angalau

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
		(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 41(1)(c))			Miongoni mwa masharti hayo ni mtoa huduma wa usafiri ardhini mwenye vyombo vya usafiri chini ya sita kuwa na mtumishi mwenye angalau "*level six of national technical award on logistics and transport management*" kutoka taasisi inayotambulika. **<u>Tatizo</u>** Kanuni inataka mtoa huduma mwenye vyombo vya usafiri chini ya sita kuwa na mtumishi mwenye angalau *level six of a national technical award on logistics and transport management* kutoka	*level six of a national technical award on logistics and transport management* kutoka taasisi inayotambulika.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					taasisi inayotambulika. Masharti hayo hayana uhalisi kwa watoa huduma za usafiri wa pikipiki za matairi mawili/matatu, teksi, kukodi, *ride-hailing service* na *ride sharing* kwakuwa, yamezingatia idadi vya vyombo. Masharti hayajazingatia upatikanaji wa kipato kutokana na shughuli zinazoendeshwa na mtoa huduma. Hali inaweza kusababisha ugumu wa kukidhi mahitaji ya kisheria ya aliyeajiriwa (mshahara na stahili nyingine).	

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					2. **Kanuni ya 12** inahusu masharti ya kuendesha shughuli za usafirishaji kama kampuni au ushirika. **<u>Tatizo</u>** Inamtaka mtoa huduma kuwa na mabasi yasiyopungua manne. Masharti ya Kanuni hii yanaweza kutafsiriwa kuwa ni kikwazo katika biashara kwakuwa yanazuia ukuaji watoa huduma wadogo wanaoendesha shuguli za usafiri hizo pasipo kuwa na mabasi zaidi ya manne.	2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha mazingira yanayoweza kuruhusu mtoa huduma aliye na chini ya mabasi manne kutoa huduma ya usafiri kwa umbali unaozidi kilometa 600.
9.	**TS Na. 16** 12 Januari, 2024	*Rules under the Land Transport Regulatory*	*The Land Transport*	Wizara ya Uchukuzi	1. **Kanuni ya 6** inaanzisha Kamati ya	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha idadi ya

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
		Authority (Complaint Handling Procedures), 2024 **(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 41(1)(d))**	*Regulatory Authority Act, (Cap. 413)*		Kushughulikia Malalamiko. **<u>Tatizo</u>** Kanuni ina dosari ya kutoonesha: - i) idadi ya Wajumbe wanaounda Kamati; ii) taaluma inayohitajika kuteuliwa kwa mjumbe wa Kamati; na iii) akidi ya vikao vya Kamati 2. **Kanuni ya 8** imeweka utaratibu kwa mteja kuwasilisha malalamiko yake kwa mtoa huduma.	wajumbe wa Kamati; taaluma ya Wajumbe na akidi ya vikao vya Kamati 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kuwa, njia itakayotumika kuwasilisha malalamiko kwa njia ya maandishi.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Kanuni hazioneshi njia itakayotumika kuyawasilsha malalamiko yanayohusika. Kutokuanishwa kwa njia hiyo ni doasri inayokwamisha madhumuni ya sheria ndogo ambayo ni kufafanua utekelezaji wa sheria mama. Aidha, inakanganya walengwa wa sheria ndogo katika suala la uwasilishaji wa malalamiko jambo ambalo ni kinyume na lengo la Bunge kukasimu madaraka ya kuweka kanuni.	
10.	**TS Na. 28** 15 Disemba, 2023	Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmshauri ya	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	1. **Kifungu cha 6 (2) k**inaweka masharti kuhusu muda wa kukusanya ada na	1. **Kifungu cha 6 (2)** kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa ya maneno

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
		Wilaya ya Geita ya Mwaka 2024 **(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))**	(Sura ya 290)		ushuru baada ya muda uliopangwa. **<u>Tatizo</u>** Kifungu kina makosa ya uandishi kwa kutumia neno "**bila Kujali**" badala ya neno "**bila kuathiri**". Makosa hayo ya uandishi yanayeyusha uzito wa masharti yanayotangulia. 2. **Kifungu cha 13** kinahusu Ulipaji wa gharama za kuhifadhi mzigo au chombo kilichokamatwa **<u>Tatizo</u>** Kifungu kuweka sharti la kutoza malipo ya asilimia tano kwa	**bila kujali** na badala yake kuweka maneno **bila kuathiri.** 2. **Kifungu cha 13** kifanyiwe marekebisho ili kufuta tozo ya asilimia 5 ya gharama ya chombo na badala yake kuweka sharti la kutoza ya gharama za kuhifadhi chombo hicho.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					chombo kilichobeba mzigo, badala ya kutoza mzigo ambao haujalipiwa ushuru. Aidha, sharti la Halmashauri kuuza chombo kwa kushindwa kulipiwa kwa muda wa siku saba inaweza kutafsiriwa kuwa uonevu. 3. Mpangilio wa sheria ndogo umegawanywa katika Sehemu ambazo zinazungumzia masuala mbalimbali. **<u>Tatizo</u>** Sheria ndogo ina makosa ya uandishi kwakuwa na Sehemu ya Pili tu. Kukosekana	3. Sheria Ndogo ifanyiwe marekebisho kwa kufuta kichwa cha Habari cha sehemu ya pili.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					kwa sehemu nyingine kunasababisha kukosekana kwa ufafanuzi unaokusudiwa.	
11.	**TS Na. 29** 12 Januari, 2024	Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, 2023 **(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 6(1) na 16(1))**	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura ya 290)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	1. **Kifungu cha 12** kinahusu Ulipaji wa gharama za kuhifadhi mzigo au chombo kilichokamatwa **<u>Tatizo</u>** Kifungu kuweka sharti la kutoza malipo ya asilimia tano kwa chombo kilichobeba mzigo, badala ya kutoza mzigo ambao haujalipiwa ushuru. Aidha, sharti la Halmashauri kuuza chombo kwa kushindwa kulipiwa kwa muda wa siku saba inaweza	1. **Kifungu cha 12** kifanyiwe marekebisho ili kufuta tozo ya asilimia 5 ya gharama ya chombo na badala yake kuweka sharti la kutoza ya gharama za kuhifadhi chombo hicho.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni

					kutafsiriwa kuwa uonevu.
					
					2. **Sehemu ya Kumi na Sita ya Jedwali la Kwanza** inahusu Ada ya Shughuli za Burudani, Utamaduni, Sanaa na Matangazo.
					
					Katika sehemu hii, kuanzia **kipengele cha 16 hadi cha 22** vinainisha viwango mbalimbali kama ifuatavyo:-
					
					i) Udhamini wa vipindi, filamu na tamthilia 755,000/= kwa dakika 30 hadi 35;
					
					ii) Taarifa ya Habari 2,500,000/= kwa siku 30;
						2. Sheria ndogo ifanyiwe marekebisho ili kuweka bayana kuwa malipo hayo yanahusu Televisheni ya Halmashauri.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni

					iii) Maandishi kupita sauti 10,000/= kwa sekunde 60;
					
					iv) Picha 300,000/= kwa sekunde 60;
					
					v) Picha1,000,000/= kwa siku 7 (Picha nyingine);
					
					vi) Mahojiano 250,000/= kwa dakika 30; na
					
					vii) Matangazo ya kampuni mbalimbali asubuhi, mchana na jioni 3,000,000/= kwa sekunde 60.
					
					<u>Tatizo</u>
					Kipengele cha 16 hadi cha 22	

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					vinavyoweka viwango mbalimbali, haviweki bayana masharti kuhusu utozaji na ulipaji wa viwango hivyo kutokana na kutobainisha ipasavyo vinavyozingatiwa katika utozaji na wanaostahili kulipa (iwapo ni mtazamaji? au mtangazaji? au mmiliki wa chombo? au mtoa tangazo?). Jambo hili linazikosesha sheria ndogo hizo uwezo wa kufanikisha lengo la Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 ambalo ni pamoja na kuwezesha ukusanyaji bora wa	

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					fedha katika mamlaka ya Serikali za Mita 3. **Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Kwanza** inaweka viwango vya ushuru wa madini ya ujenzi. **<u>Tatizo</u>** Viwango vya shilingi 150,000/- kwa miezi sita na shilingi 300,000/- kwa mwaka vinaathiri ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri, kwakuwa ni vidogo na havina uwiano mzuri ikilinganishwa na bei ya tripu moja na idadi ya tripu zinazoweza kubebwa kwa siku.	3. Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Kwanza ifanyiwe marekebisho ili kuweka viwango vyenye uwiano na uhalisia.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
12.	**TS Na. 30** 12 Januari, 2024	Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, 2024 **(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 89)**	Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), (Sura ya 288)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	1. **Kifungu cha 3** cha sheria ndogo kinatafsiri maneno mbalimbali yaliyotumika katika sheria ndogo ikiwemo kifungu cha maneno **taka ngumu** **<u>Tatizo</u>** Tafsiri ya kifungu cha maneno **taka ngumu katika Kifungu cha 3 cha sheria ndogo** inafautiana na tafsiri ya **taka ngumu** iliyo katika **Kifungu cha 3** Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Hali hi:- i) Inaifanya sheria ndogo hii ikinzane na sheria ya Bunge; na	1. Kifungu cha 3 kifanyiwe marekebisho ili kuweka tafsiri ya taka ngumu kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					ii) Inaweka uwezekano wa lengo la sheria ndogo hii kutofikiwa. 2. **Kifungu cha 5 (e)** kinaweka wajibu wa kila mtu mwenye mamlaka ya usimamizi wa jengo kuhakikisha kwamba kunakuwa na choo bora. **<u>Tatizo</u>** Kifungu hakioneshi maana ya Kifungu cha maneno "choo bora" wala kutaja vigezo vipi vitakavyotumiwa na Halmashauri katika kuuamua ubora wa choo.	2. **Kifungu cha 5 (e)** kifanyiwe marekebisho ili kutaja sifa za choo bora.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					Hali hii inakosesha utoshelevu wa ufafanuzi unaotolewa na sheria ndogo kwakuwa inategemeza tafsiri kwenye mtazamo wa msimamizi na mtekelezaji. 3. **Kifungu cha 7** kinahusu udhibiti wa kelele kwa shughuli mbalimbali za kijamii. **<u>Tatizo la Kwanza</u>** Kifungu kimeweka sharti kwa mtu yeyote anayetaka kutumia kangavuke kupata kibali cha Halmashauri. Masharti yaliyoweka na Kifungu hiki hayaoneshi muda	3. Sheria ndogo ifanyiwe marekebisho kwa kufuta **Kifungu cha 7** na badala yake Halmashauri itumie Sheria ya Mazingira na Kanuni za Ujenzi Mijini ambazo zinaelekeza utaratibu wa kuzuia kelele.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					wa kibali hicho kutumika kama ni siku, wiki, mwezi, mwaka au kipindi cha muda wa kutumia Kangavuke na mazingira yanayosababisha kuomba kutumia kangavuke. Uwekaji huo wa masharti kwa namna ulivyo, unaleta mkanganyiko miongoni mwa wasimamizi na walengwa wa kifungu hicho na hivyo kutokidhi dhima ya kufafanua utekelezaji wa sheria mama na sheria nyingine za nchi.	

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo la Pili</u> Kifungu kinaelekeza kupata kibali cha Halmashauri kwa kitu kingine chochote pasipo kubainisha kitu kinachohusika. Maelekezo hayo yalivyowekwa bila kuwa na mipaka ya mambo yanaweza:- i) Kugusa upana mkubwa usiokusudiwa na sheria ndogo hii au kutoka nje ya wigo wa mambo yaliyokusudiwa; ii) Kutafsiriwa hadi kwenye mambo mengine yanayowekewa utaratibu na sheria nyingine	

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					ikasababisha ukinzani au mkanganyiko. Athari hizo zinaweza kuonekana kuwa dosari kubwa katika uhakika unaosthili kuwekwa na sheria. (Uhalisia) 4. **Kifungu cha 13** inahusu masharti ya utengenezaji na uzaji vyakula **<u>Tatizo</u>** Kanuni ya 13 kinajumuisha wasio wafanya biashara kukaguliwa nyumbani kwao ikiwa wametimiza kanuni za afya ikiwemo wakati wa kuchemsha na kupika chakula.	4. **Kifungu cha 13** cha Sheria Ndogo kifanyiwe marekebisho ili kubainisha na kutofautisha watu ambao wataguswa na Sheria Ndogo hii.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					5. **Kifungu cha 32(1)(f)** kinaweka katazo la kupiga picha katika fukwe pasipo kibali. **<u>Tatizo la Kwanza</u>** Sheria ndogo haijataja fukwe zinazokusudiwa. **<u>Tatizo la Pili</u>** Hitaji la kibali cha Halmashauri ili kupiga picha ufukweni linanyima wananchi haki ya matumizi ya fukwe.	5. Sheria ndogo ifanyiwe marekebisho kwa kufuta Kifungu cha **32(1)(f)** ili kuondoa sharti la kupiga picha katika fukwe pasipo kibali.
					6. **Kifungu cha 14** kinaweka sharti kwa wauzaji wa chakula kutumia masanduku ya mbao yaliyo na vioo kuhifadhia chakula.	6. **Kifungu cha 14** kifanyiwe marekebisho ili kutambua aina nyingine za masanduku ya kuhifadhia chakula.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Kifungu kimeweka sharti la matumizi ya masanduku ya mbao yenye vioo kuhifadhia chakula pasipo kuzingatia masanduku ya aina nyingine.	
13.	**TS Na. 38** 19 Januari, 2024	Sheria Ndogo ya (Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 **(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))**	Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	1. **Kifungu cha 3** kinaweka tafsiri ya maneno mbalimbali, ambapo pamoja na maneno mengine, imetafsiri neno **"mfugo"** kuwa ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, na wanyama wengine wafugwao na binafsi. **<u>Tatizo</u>** Neno "**binafsi"** limetumika bila mantiki na hivyo kutatiza tafsiri ya	1. **Kifungu cha 3** kifanyiwe marekebisho kwa kufuta neno "binafsi" ili kuleta maana iliyokusudiwa.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					neno **"mfugo"** iliyokusudiwa na sheria ndogo na kukwamisha utekelezaji wa sheria ndogo. 2. **Kifungu cha 3** kimeweka tafsiri ya neno Mkurugenzi **<u>Tatizo</u>** Kifungu kina makosa ya uandishi kwa kutafsiri Mkurugenzi kuwa ni **Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Moshi** badala ya **Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.** 3. **Kifungu cha 22** kinahusu udhibiti wa ufugaji mbwa	2. **Kifungu cha 3** cha Sheria Ndogo kifanyiwe marekebisho kwa kuongeza neno "Halmashauri" ili kuleta maana iliyokusudiwa. 3. **Kifungu cha 22** kifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Kifungu kina makosa ya uandishi kwa kutumia neno "***hatakaye ruhusiwa***" ambalo halina maana na linakanganya masharti kuhusu udhibiti wa ufugaji mbwa na kupoteza mantiki iliyokusudiwa. 4. **Kifungu cha 26** kinataja makosa mbalimbali yanayokatazwa na sheria ndogo hii ikiwemo, kosa kwa mtu yeyote kufanya shughuli za kisiasa ikiwa ni pamoja na kupandisha bendera ya Chama cha Siasa.	"hatakaye ruhusiwa" na badala yake kuweka neno "hataruhusiwa". 4. Kifungu kifanyiwe marekebisho kwa kufuta Kifungu cha 26(s).

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> **Kifungu cha 26 (s)** kinakataza kufanya shughuli za kisiasa na kupandisha bendera za vyama za siasa pasipo kufafanua maeneo yaliyowekwa katazo la kufanya shughuli hizo. Masharti ya Kifungu hiki yanaleta athari kubwa katika sheria ikiwa ni pamoja na:- i) Kutafsirika kuwa katazo kwa watu wote kufanya shughuli za kisiasa ambayo ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;	

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					ii) Kukiuka masharti yaliyowekwa na Sheria ya Vyama vya Siasa; iii) Kuvuka mipaka inayostahili kutokana na madhumuni ya kutunga sheria yaliyokusudiwa. 5. **Kifungu cha 10(4)** kinaweka sharti kwa Halmashauri kumjulisha mmiliki kabla ya kuuza mfugo uliokamatwa. **<u>Tatizo</u>** Kifungu hakioneshi masharti ya kipindi cha muda wa kumjulisha mmiliki kabla ya kuuza mifugo (siku, wiki,	5. **Kifungu cha 10(4)** cha Sheria Ndogo kifanyiwe marekebisho ili kuainisha muda wa kumpa taarifa mmiliki wa mfugo kabla ya mfugo wake kuuzwa.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					mwezi au mwaka). Hivyo Kifungu kinaacha ombwe la sharti la muda ,jambo linaloweza kutatiza utekelezaji au kuacha mianya ya kutumika vibaya kutokana na kutoweka uhakika na kutabirika kwa sheria.	
14.	**TS Na. 39** 19 Januari, 2024	Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 **(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))**	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura ya 290)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	1. **Kifungu cha 8(1)(a)** inahusu ushuru wa mazao. **<u>Tatizo</u>** Kifungu kina makosa ya uandishi kwa kurudia maudhui ya aya (a) katika aya (b). 2. **Jedwali la Kwanza** linahusu utozaji wa ada au ushuru kwa	1. **Kifungu cha 8** kifanyiwe marekebisho kwa kufuta aya ya **(b)** iliyojirudia. 2. Marekebisho yafanyike katika:-

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					ajili ya Huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri. **<u>Tatizo la Kwanza</u>** **Sehemu ya Kwanza ya Jedwali** inaweka ada ya vibali vya burudani ya kandanda kwa viwango vya shilingi 1,000/= kwa mtu mzima, na shilingi 500/= kwa mtoto. Jedwali hilo halioneshi namna ya utozaji wake, jambo linaloacha utata kwamba itatozwa kwa burudani ya viwanjani au vibanda vya kuonesha kandanda.	i) **Jedwali la Kwanza Sehemu ya Kwanza kipengele cha 10** kwa kuongeza maneno **viwanja vya Halmashauri**. mbele ya maneno **burudani ya kandanda**; na ii) Marekebisho yafanyike katika **Jedwali la Kwanza Sehemu ya Kumi na Tatu** kwa kuongeza maneno **Mamlaka.**

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					Kutoainishwa kwa namna ya utozaji wa ushuru kunaweza kusababisha utozaji kwa kuzingatia utashi, hivyo kuathiri malengo ya ukusanyaji wa ushuru yaliyokusudiwa na sheria ndogo. **<u>Tatizo la Pili</u>** Kichwa cha Habari cha Jedwali la Kwanza Sehemu ya Kumi na Tatu kina makosa ya uandishi kwa kutumia maneno "**Ya Mapato Tanzania (TRA)**" ambayo hayajakamilika. (Jedwali) Hali hii inaweza kuleta utata na	

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					kutokueleweka kwa sheria ndogo hizi. **<u>Tatizo la Tatu</u>** Sehemu ya Ishirini ina makosa ya uandishi katika kichwa cha Habari. Hali hii inaweza kuleta utata na kutokueleweka kwa sheria ndogo hizi. 3. **Jedwali la Tatu** linahusu kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi. **<u>Tatizo</u>** Kibali kina makosa ya uandishi kwa kutaja sanduku la posta la Mlimba ilhali sheria ndogo hizi ni za Halmsahauri ya Wilaya ya Moshi.	3. **Jedwali la Tatu** lifanyiwe marekebisho kwa kufuta neno **Mlimba** na badala yake kuweka neno **Moshi.**

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
15.	**TS Na. 840** 17 Novemba, 2023	*Regulations under The Atomic Energy (Protection from Ionizing and Non-Ionizing Radiation), 2023* **(Zimetengenezwa chini ya Kifungu cha 70)**	*The Atomic Energy Act, (Cap. 188)*	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya Habari	1. **Kanuni ya 3** inatafsiri maneno mbalimbali yaliyotumika katika Kanuni. **<u>Tatizo</u>** Kanuni ina makosa ya uandishi kwa kukosa mtiririko wa kialfabeti katika maneno yaliyotafsiriwa. Hali hii inasababisha usumbufu kwa wasomaji wakati wa usomaji wa sheria ndogo. 2. **Kanuni ya 3** inaweka tafsiri ya neno *Commission* **<u>Tatizo</u>** Tafsiri ya neno *Commission* haijakamilika	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka mtiririko wa kialfabeti 2. Kanuni ya 3 ifanyiwe marekebisho ili kuonesha Kifungu cha 5 kinachorejewa katika tafsiri ya neno Commission ni cha sheria ipi.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					kutokana na kutoonesha Kifungu cha 5 kinapatikana katika sheria gani. 3. **Kanuni ya 8(1)** inaweka masharti kwamba, mtu yeyote anayekusudia kufanya jambo lililotajwa bayana katika Kanuni hizi atalazimika kuitaarifu Tume kwa namna ilivyoelekezwa na Tume. **<u>Tatizo</u>** Kanuni hazina maelezo ya utaratibu unaostahili kufuatwa katika kutekeleza masharti ya kuitaarifu Tume kuhusu kusudio la kufanya jambo	3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kubainisha utaratibu wa kutoa taarifa kuwa ni kupitia Fomu ya kutoa Taarifa ambayo itapatikana katika Jewali.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					lililobainishwa kwenye kanuni hizo na hivyo kutokamilisha ufafanuzi kwa ajili ua utekelezaji wa sheria mama. Kwa upungufu huo, lengo la kanuni kufafanua na kurahisisha utekelezaji wa sheria mama linakwama kutokana na kukosa ukamilifu katika ufafanuzi. (Uandishi) 4. **Kanuni ya 13** inahusu marekebisho, kusimamishwa kwa muda na kufutwa kwa idhini. **<u>Tatizo</u>** Kanuni imerejea Kanuni ya 8 ambayo	4. Kanuni ya 13 ifanyiwe marekebisho ili kurejea kanuni sahihi.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					maudhui yake hayahusiani na marekebisho, kusimamishwa kwa muda na kufutwa kwa idhini.	
16.	**TS Na. 889** 15 Disemba, 2023	Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, 2023 **(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))**	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura ya 290)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	**Kifungu cha 5** kinachohusu uanzishaji wa nafasi ya Mkuu wa soko na majukumu yake, kinaipa Halmashauri ya Wilaya ruhusa ya kuajili bila kujali kuwepo kwa Mkuu wa soko. **<u>Tatizo</u>** **Kifungu cha 5(2)** kinafifisha wadhifa ulioanzishwa katika Kifungu cha 5(1) kutokana na matumizi ya maneno "**bila Kujali**" badala ya neno "**bila kuathiri**". Kwa ufifishaji huo wa masharti na kifungu	**Kifungu cha 5** kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa maneno bila kujali na badala yake kuweka maneno **bila kuathiri.**

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					chenyewe, sheria ndogo hizo zinakanganya badala ya kusaidia utekelezaji wa sheria mama hususan masuala ya ushuru wa masoko na magulio.	
17.	**TS Na. 907** 22 Disemba, 2023	Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, 2023 **(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))**	Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	1. **Kifungu cha 7(4)** kinaweka sharti kwa Halmashauri kumjulisha mmiliki na umma kabla ya kuuza mfugo uliokamatwa. **<u>Tatizo</u>** Kifungu hakioneshi masharti ya kipindi cha muda wa kumjulisha mmiliki kabla ya kuuza mifugo (siku, wiki, mwezi au mwaka). Hivyo Kifungu	1. **Kifungu cha 7(4)** cha Sheria Ndogo kifanyiwe marekebisho ili kuainisha muda wa kumpa taarifa mmiliki wa mfugo kabla ya mfugo wake kuuzwa.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					kinaacha ombwe la sharti la muda ,jambo linaloweza kutatiza utekelezaji au kuacha mianya ya kutumika vibaya kutokana na kutoweka uhakika na kutabirika kwa sheria. 2. **Kifungu cha 11(1)(a)** kinaweka katazo la kufanya shughuli za kilimo katika maeneo yenye miteremko. **<u>Tatizo</u>** KIfungu kimeweka katzao la jumla pasipo kuonesha ruhusa ya kulima kwa kuzingatia kanuni za kilimo kwenye miteremko au miinuko.	2. **Kifungu cha 11(1)(a)** kifanyiwe marekebisho kwa kuongeza maneno **ruhusa ya kulima kwa kuzingatia kanuni za kilimo kwenye maeneo ya miteremko na miinuko**.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
18.	**TS Na. 908** 22 Disemba, 2023	Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, 2023 **(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))**	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura ya 290)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	1. **Kifungu cha 5** kinahusu kuanzishwa kwa nafasi ya mkuu wa soko anayeteuliwa na Halmashauri ili kusimamia shughuli za soko. **<u>Tatizo</u>** **Kifungu cha 5(3)** kinafifisha wadhifa ulioanzishwa katika Kifungu cha 5(2) kutokana na matumizi ya maneno "**bila Kujali**" badala ya neno "**bila kuathiri**". Kwa ufifishaji huo wa masharti na kifungu chenyewe, sheria ndogo hizo zinakanganya badala ya kusaidia	1. **Kifungu cha 5** kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa maneno bila kujali na badala yake kuweka maneno **bila kuathiri.**

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					utekelezaji wa sheria mama hususan masuala ya ushuru wa masoko na magulio. 2. **Kifungu cha 7** kinahusu majukumu ya Kamati. **<u>Tatizo</u>** Aya (g) imetumia neno **Mkuu wa Masoko** badala ya Mkuu wa soko ammbaye ndiye ametafsiriwa katika Kifungu cha 3. 3. **Jedwali la Tatu** linahusu kibali cha kutumia soko. **<u>Tatizo</u>** Sheria ndogo ina makosa ya uandishi	2. **Kifungu cha 7 aya (g)** kifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno **mkuu wa masoko** na badala yake kuweka maneno **mkuu wa soko.** 3. **Jedwali la Tatu** lifanyiwe marekebisho kwa kubadilisha namba katika Jedwali la kufifilisha kosa.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					kwa kuwa na Jedwali jingine la Tatu linalohusu Hati ya Kufifilisha kosa. 4. **Jedwali la Tatu** linahusu Hati ya Kufifilisha Kosa. **<u>Tatizo</u>** Hati inamtaja Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ilhari sheria ndogo zinazohusika zipo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba.	4. **Jedwali la Tatu** lifanyiwe marekebisho kwa kufutaa neno **Rorya** na badala yake kuweka neno **Mlimba..**
19.	**TS Na. 917** 22 Disemba, 2023	Sheria Ndogo Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, 2023	Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	**Kifungu cha 9(3)** kinaweka sharti kwa Halmashauri kumjulisha mmiliki kabla ya kuuza mfugo uliokamatwa.	**Kifungu cha 9(3)** cha Sheria Ndogo kifanyiwe marekebisho ili kuainisha muda wa kumpa taarifa mmiliki wa mfugo kabla ya mfugo wake kuuzwa.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
		(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))			**<u>Tatizo</u>** Kifungu hakioneshi masharti ya kipindi cha muda wa kumjulisha mmiliki kabla ya kuuza mifugo (siku, wiki, mwezi au mwaka). Hivyo Kifungu kinaacha ombwe la sharti la muda ,jambo linaloweza kutatiza utekelezaji au kuacha mianya ya kutumika vibaya kutokana na kutoweka uhakika na kutabirika kwa sheria.	
20.	**TS Na. 918** 22 Disemba, 2023	Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 **(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))**	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura ya 290)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	1. **Kifungu cha 3** cha sheria ndogo hizi kinaweka tafsiri za maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya sheria ndogo. **<u>Tatizo</u>** Kifungu kimetafsiri neno Mkurugenzi wa	1. **Kifungu cha 3** kifanyiwe marekebisho kwa kufuta neno **Biharamulo** na badala yake kuweka neno **Kibondo.**

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilhali sheria ndogo hizi zipo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo. (Uandishi) 2. **Kifungu cha 7** kinahusu muda wa kukusanya ada na ushuru. **<u>Tatizo</u>** Maudhui ya Kifungu kidogo cha (2) na (5) yanafanana, hivyo kuleta utata katika kufanya rejea ya Kifungu. 3. **Sehemu ya Tatu ya Jedwali** inahusu ushuru wa matangazo au sanaa au tamasha.	2. **Kifungu cha 3** kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa maudhui yanayojirudia. 3. Shemu ya Tatu ya Jedwali ifanyiwe marekebisho kwa kuweka viwango vyenye uwiano na

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Kipengele nane kimewekewa ushuru wa ada za kumbi za starehe na mikutano kuwa ni shilingi 25,000 kwa siku pasipo kufafanua unalipwaji huo ni kwa siku ya tukio la sherehe au kila siku hata kama hakuna tukio katika ukumbi uhaohusika.	uhalisia kwa kuzingatia matukio.
21.	**TS Na. 919** 22 Disemba, 2023	Sheria Ndogo ya Kuzuia Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 **(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1)(b))**	Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	**Kifungu cha 16** kinahusu makosa na adhabu **<u>Tatizo</u>** **Aya (c)** inatoa adhabu kwa mtu yeyote atakayeshindwa kuondoa kwa wakati mazao shambani baada ya kuvuna. Adhabu inayowekwa na Kifungu hiki haina uhalisia kwa haizingatii	Kifungu cha 16 kifanyiwe marekebisho ili kuonesha kuwa mtu atakuwa ametenda kosa iwapo atashindwa kuondoa mazao baada ya kuvuna bila kuwa na sababu za msingi.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					sababu za msingi zinazoweza kumzuia mtu kuondoa mazao shambani.	
22.	**TS Na. 920** 22 Disemba, 2023	Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 **(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))**	Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	**Kifungu cha 16 (e)** cha sheria ndogo hii kinaweka katazo kwa mtu yeyote aliye ndani ya gari kudondosha taka ngumu nje ya gari likiwa ndani au nje ya kituo cha magari na sehemu yoyote ile ambapo gari hilo linapita. **<u>Tatizo</u>** Sheria ndogo hii imekataza utupaji wa taka ngumu peke yake bila kujumuisha taka laini na nyinginezo. Kutokutajwa kwa taka laini na nyinginezo kunaweza kuleta tafsiri ya ruhusu ya kutupa	**Kifungu cha 16 (e)** kifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno **taka ngumu** na badala yake kuweka neno **taka** kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					taka hizo, hivyo kuathiri lengo la sheria ndogo hizi na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira zenye lengo la kuweka mazingira katika hali ya usafi na usalama.	
23.	**TS Na. 921** 22 Disemba, 2023	Sheria Ndogo ya Usafi, Afya na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, 2023 **Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))**	Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	1. **Kifungu cha 3** cha sheria ndogo kinatafsiri maneno mbalimbali yaliyotumika katika sheria ndogo ikiwemo kifungu cha maneno **taka ngumu** **<u>Tatizo</u>** Tafsiri ya kifungu cha maneno **taka ngumu katika Kifungu cha 3 cha sheria ndogo** inafautiana na tafsiri ya **taka ngumu** iliyo katika **Kifungu cha 3** Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.	1. **Kifungu cha 3** cha kifanyiwe marekebisho kwa kufuta tafsiri ya maneno **taka ngumu** na badala yake kuweka tafsiri iliyopo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					Hali hi:- i) Inaifanya sheria ndogo hii ikinzane na sheria ya Bunge; na ii) Inaweka uwezekano wa lengo la sheria ndogo hii kutofikiwa. (Sheria nyingine) 2. **Kifungu cha 8** kinaweka sharti kwa mtu yoyote anayetaka kujenga choo cha watu wenye mahitaji maalum kuzingatia masharti atakayopewa na Halmashauri.	2. **Kifungu cha 8** kifanyiwe marekebisho kwa kuweka masharti ya kuzingatia ili kujenga choo cha watu wenye mahitaji maalum.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					Tatizo Kifungu hakibainishi masharti yanayostahili kuzingatiwa na mtu anayetaka kujenga choo cha watu wenye mahitaji maalum hakijaweka bayana ni masharti yapi yanayotolewa endapo mtu anataka kujenga choo cha watu wenye mahitaji maalum. Kutobainisha masharti hayo ni kuipa Halmashauri kuweka masharti kwa idadi na namna isiyojulikana au isiyo na ukomo. Hali hiyo inamruhusu msimamizi wa sheria ndogo kuamua	

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					masharti kadri atakavyoona yeye kwa wakati tofauti. 3. **Kanuni ya 11(4)** inazungumzia kuhusu kutupa au kutekeleza taka hatarishi kwa kuzingatia taratibu za utupaji wa taka hizo. **<u>Tatizo</u>** Kifungu hakijaweka wazi utaratibu unaopaswa kuzingatiwa. Kutokutajwa kwa utaratibu huo, kunasababisha kutokueleweka kwa uzingatiaji wa masharti miongoni mwa walengwa wa sheria ndogo hizi.	3. **Kifungu cha 11(4)** kifanyiwe marekebisho ili kufafanua utaratibu unaopaswa kufuatwa wakati wa kutupa au kuteketeza taka hatarishi.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					4. **Kifungu cha 25(6)** kinaweka sharti kwa Halmashauri kumjulisha mmiliki kabla ya kuuza mfugo uliokamatwa. **<u>Tatizo</u>** Kifungu hakioneshi masharti ya kipindi cha muda wa kumjulisha mmiliki kabla ya kuuza mifugo (siku, wiki, mwezi au mwaka). Hivyo Kifungu kinaacha ombwe la sharti la muda, jambo linaloweza kutatiza utekelezaji au kuacha mianya ya kutumika vibaya kutokana na kutoweka uhakika na kutabirika kwa sheria.	4. **Kifungu cha 25(6)** kifanyiwe marekebisho ili kuainisha muda wa kumpa taarifa mmiliki wa mfugo kabla ya mfugo wake kuuzwa.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					5. **Kifungu cha 26(2)** kinahusu udhibiti wa sauti na mitetemo. **<u>Tatizo</u>** Kifungu kinaweka sharti la lazima la kuweka sauti isiyoleta kero kwa majirani, pasipo kuonesha kiwango cha sauti siyo na kero. 6. **Jedwali la Nne** linaonesha viwango vya malipo ya ukaguzi, usajili, kupima afya na kupulizia dawa ya kuua wadudu waenezao magonjwa kwa binadamu.	5. **Sheria Ndogo** ifanyiwe marekebisho kwa kufuta **Kifungu cha 26(2)** na badala yake itumike Sheria ya Mazingira na Kanuni za Ujenzi Mijini ambazo zinaelekeza utaratibu wa kuzuia kelele. 6. Jedwali la Nne lifanyiwe marekebisho **kufuta kichwa cha habari cha Jedwali la Nne** na kukiandika upya.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<u>Tatizo</u> Jedwali halioneshi viwango vya malipo ya usajili kama ilivyooneshwa katika kichwa cha habari cha Jedwali. Hali hiyo inatatiza walengwa na wasimamizi wa sheria jambo linalozuia kufikiwa kwa lengo la sheria ndogo kuhusu kuwezesha utekelezaji wa sheria mama.	
24.	**TS Na. 926** 29 Disemba, 2023	*Rules under the College of Business Education (Examinations)*, 2023 **(Zimetungwa chini ya Kifungu 14(1))**	*The College of Business Education* (Cap. 315)	Wizara ya Viwanda na Bisahara	1. **Kanuni ya 3** inatafsiri maneno mbalimbali likiwemo *abscondmnent*. **<u>Tatizo</u>** Kanuni inaelekeza iwapo mwanafunzi hatakuwepo chuoni atapaswa kupata	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kutambua mazingira ya dharura kumzuia mwanafunzi kuhudhuria chuo pasipo kuwa amepata ruhusa ya awali.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					ruhusa ya awali (*prior permission*). Tafsiri haijatambua mazingira ya dharura yanayoweza kumzuia mwanafunzi kuhudhuria chuo pasipo kuwa amepata ruhusa ya awali. 2. **Kanuni ya 32(6)** inaipa Chuo mamlaka ya kutangaza katika chombo cha habari cha umma jina na picha ya mwanafunzi aliyepatikana na hatia ya kukiuka taratibu za mitihani. Mamlaka hayo yanaweza kutafsirika kuwa adhabu isiyozingatia mantiki na madhara	2. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa takwa la kutangazwa katika chombo cha habari cha umma jina na picha ya mwanafunzi aliyepatikana na hatia ya kukiuka taratibu za mitihani.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					ikilinganishwa na ukubwa wa kosa. Hali hiyo inaweza kuonekana kuwa utekelezaji wa sheria ya Bunge Sura 315 haujali madhara makubwa ya adhabu ya kosa lisilo na ukubwa unaowiana na madhara haya. 3. **Kanuni ya 45** inazungumzia kuhusu utaratibu wa Kamati ya Rufaa ya Matokeo ya Mitihani kushughulikia rufaa za kupinga matokeo ya mitihani. **<u>Tatizo la Kwanza</u>** Kanuni inakataza kukata rufaa dhidi ya tathmini endelevu.	3. Marekebisho yafanyike kwa kuongeza tathmini endelevu (course work) kuwa ni sababu ambayo mwanafunzi anaweza kukata rufaa.

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					Kanuni haijazingatia kwamba, matokeo ya mtihani yanayoruhusiwa kukatiwa rufaa yanajumisha tathmini endelevu. **<u>Tatizo la Pili</u>** i) Kanuni haioneshi muda ambao Kamati itashughulikia rufaa; ii) Kanuni haioneshi namna ya uwasilishaji wa rufaa; na iii) Haioneshi utaratibu utakaotumika kushughulikia rufaa.	

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					Mambo hayo yanazuia ufanisi katika uzingatiaji wa misingi ya utoaji haki kutokana na: i) Kuchelewesha mchakato wa utoaji haki; ii) Kukanganya katika namna ya uwasilishaji wa rufaa; na iii) Kutoa ufafanuzi usiotosheleza katika utaratibu wa rufaa. 4. Kanuni hizi kwa ujumla zinahusu utaratibu wa mifumo ya upimaji ikiwemo pamoja na mambo mengine namna ya	4. Kanuni zifanyiwe marekebisho kwa kuainisha mazingira ya kumsikiliza mwanafunzi ambaye alishindwa kufika

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Jina la Sheria Mama	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
		vipindi tofauti vya mwaka mmoja. Hali hii inaweza kuleta madhara kwa walio na Leseni zilizopatikana kwa vipindi tofauti kwa mwaka kuisha kwa wakati wakati mmoja			
		9. **Kanuni ya 31(2)** inaweka masharti kwa mzambazaji aliyesajiliwa kutunza na kuhuisha kumbukumbu za usambazaji na uuzaji wa viuatilifu. **Kanuni 31(2) (e)** inamtaka msambazaji kutunza kumbukumbu ya taarifa nyingine yoyote kama	9. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa sharti la kumtaka msambazaji kutunza kumbukumbu ya taarifa nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na mamlaka.	9. Marekebisho yamefanyika kwa kufuta **Kanuni ya 31(2)(e)**.	9. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 3 Mei, 2024 (TS Na. 344).

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		itakavyoelekezwa na mamlaka. **<u>Tatizo</u>** Kanuni inaweka sharti la kutunza nyaraka nyingine yoyote bila kutaja nyaraka hizo. Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa			
		10. **Kanuni ya 33(2)** inazungumzia kuhusu maombi ya kibali cha unyunyiziaji wa viautilifu kwa njia ya anga, kuwa maombi hayo yanapaswa kuambatishwa na nyaraka zilizoainishwa katika katika aya (a) hadi (e).	10. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuzitaja bayana Mamlaka ya Usafiri wa Anga na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu	10. Azimio la Bunge halijatekelezwa. Wizara ilitoa maelezo kwamba, marekebisho hayajafanyika kwa sababu Mamlaka zinazohusika na utoaji wa vibali vya unyunyiziaji kutokea angani ni zaidi ya zile zilizoainishwa	10. Azimio la Bunge litekelezwe ndani ya miezi miwili na liwasilishwe katika vikao vya mwezi Novemba, 2024.

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<u>Tatizo</u> Aya (e) inaweka sharti la kupata kibali cha kifaa anga cha unyunyiziaji kutoka kwa Mamlaka. Aya hii haifafanui ni mamlaka ipi inayokusidiwa kutoa kibali hicho. Hali inasababisha kutokuelewaka kwa sharti hilo.		kwenye Kanuni Aidha, kwa kutaja majina ya Mamlaka husika italazimisha mabadiliko ya Kanuni husika endapo Mamlaka hizo zitabadilishwa majina au kubadilishiwa/kuha mishiwa majukumu yake	
		11. **Kanuni ya 51(2)** inaainisha la vipimo vya sehemu ya kuhifadhia viuatilifu kwa upana na urefu. **<u>Tatizo</u>** Kanuni haianishi vipimo vipimo vya urefu (*height*) vya sehemu ya kuhifadhia viauatilifu.	11. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la vipimo vya urefu (*height*) vya sehemu ya kuhifadhia viauatilifu.	11. Azimio la Kamati halijatekelezwa **<u>Maelezo</u>** Wizara imeeleza kuwa Kanuni ya 51(2) imefanyiwa marekebisho kwa kufuta kipengele 51(2) na kukiandika upya kikielekeza kwamba vipimo	11. Azimio la Bunge litekelezwe ndani ya miezi miwili na liwasilishwe katika vikao vya mwezi Novemba, 2024 kwa kuonesha vipimo vinavyohusika katika Jedwali la Kanuni hizi.

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		Kutokuwekwa kwa vipimo vya urefu kunaweza kuleta changamoto ya utekelezaji wa masharti ya Kanuni hivyo kuleta usumbufu kwa wanaoguswa na Kanuni hizi.		vitapatikana kwenye Miongozo.	
		12. **Kanuni ya 55 (3) (a) (b)** ina makosa ya kiuandishi. **<u>Tatizo</u>** Kanuni imetumia neno "*save*" badala ya neno "*serve*".	12. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa makosa ya kiuandishi.	12. **Kanuni ya 55(3) (a)(b)** imefanyiwa marekebisho kwa kuondoa neno "save" na kuweka neno "serve" ili kuleta maana iliyokusudiwa.	12. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 3 Mei, 2024 (TS Na. 344).
		13. **Kanuni ya 95(1)** na **Kanuni ya 97(2)** zinarejea majedwali la hamsini na moja pamoja na hamsini na saba.	13. Kanuni zifanyiwe marekebisho ili kurejea Majedwali sahihi.	13. **Kanuni ya 95(1)** imefanyiwa marekebisho kwa kuondoa neno "fiftyfirst" na kubaki na neno "first schedule" ili kuleta	13. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 3 Mei, 2024 (TS Na. 344).

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<u>Tatizo</u> Majedwali yanayorejewa na Kanuni hizi hayapo katika Kanuni hizi		maana iliyokusudiwa. Aidha, Kanuni ya 97(2) imefanyiwa marekebisho kwa kuondoa maneno "fifty- seventh" na kuweka neno "second" ili kuleta maana iliyokusudiwa.	
		14. **Kanuni ya 117 (1)** inayohusu haki ya kukata rufaa kwa mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa mamlaka, inamtaka mtu huyo kukata rufaa kwa maandishi kwa Waziri ndani ya siku 30. **<u>Tatizo</u>** Kanuni haijitoshelezi kwa ufafanuzi wa	14. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuonesha kuwa siku thelathini zitahesabika kuanzia tarehe ya kupokea nakala ya uamuzi.	14. **Kanuni ya 117(1)** imefanyiwa marekebisho kwa kuonyesha kwamba siku thelathini za kukata rufaa zitaanza kuhesabiwa tangu tarehe ya muhusika kupokea uamuzi.	14. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 3 Mei, 2024 (TS Na. 344).

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		hesabu ya siku thelathini za rufaa. Hali hii inaweza kusababisha kutokueleweka vizuri kwa haki ya kukata rufaa. 15. **Kanuni ya 114(d)** imempa Waziri mamlaka ya kumsimamisha kazi mkaguzi kwasababu ambazo Waziri anaamini kwamba zinasababisha Mkaguzi kushindwa kutekeleza kazi zake. **<u>Tatizo</u>** Kanuni zimempa Waziri kuamua kwa utashi wake, hali inayoweza kusababisha matumizi	15. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta Kanuni ya 114(d)	15. Marekebisho yamefanyika kwa ku futa Kanuni ya 114(d).	15. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 3 Mei, 2024 (TS Na. 344).

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		mabaya ya mamlaka hayo. 16. **Kanuni ya 117 (5)** inaeleza kuhusu uamuzi unaoweza kutolewa na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania baada ya kusikiliza rufaa. **<u>Tatizo</u>** Kanuni inaitaja Mamlaka kuwa ndio itatoa uamuzi wa rufaa ilhali mamlaka ndio mlalamikiwa. Hali hii ni kinyume na inayowekwa katika misingi ya haki ya asili, inayokataza mtu kuamua shauri ambalo yeye ni sehemu ya shauri hilo.	16. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta neno "*Authority*" na kuweka neno "*Minister*"	16. **Kanuni ya 117(5)** imefanyiwa marekebisho kwa kufuta neno "*Authority* "na kuweka neno "Minister".	16. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 3 Mei, 2024 (TS Na. 344).

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU)					
2.	Kanuni za Egonomia,2023 (Zimetungwa chini ya kifungu cha 109) **(TS Na. 288)** 7 Aprili, 2023	1. **Kanuni ya 5** inahusu wajibu wa wanaoweza kukumbwa na visababishi hatari za egonomia. Ambapo kanuni hii pia inaweka wajibu kwa muajiriwa. **<u>Tatizo</u>** Kuwekwa kwa wajibu wa mwajiriwa ni kinyume na **Kanuni ya 3** inayohusu wigo wa matumizi wa kanuni hizi. Hali hii inaweza kuathiri utekelezaji bora wa sheria mama.	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kumjumuisha mtu yeyote anayeweza kukumbwa na visababishi hatari vya egonomia.	1. Marekebisho ya Kanuni ya 5 yamefanyika kwa kuongeza mtu yeyote anayeweza kukumbwa na egonomia.	1. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 16 Agosti, 2024 (TS. Na. 25).
		2. **Kanuni ya 7(1)** inahusu tathmini ya athari za egonomia.	2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka tafsiri ya neno "Mamlaka"	2. Marekebisho yamefanyika katika **Kanuni ya 2** kwa	2. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<u>Tatizo</u> Kanuni imetumia "Mamlaka" pasipo kuweka tafsiri yake. Hali hiyo inasababisha kutokukamilika kwa ufafanuzi unaotarajiwa kutolewa na Kanuni hizi.		kuongeza tafsiri ya neno "Mamlaka".	Gazeti la Serikali la tarehe 16 Agosti, 2024 (TS. Na. 25)
		3. **Kanuni ya 11** inazungumzia kuhusu utunzaji wa kumbukumbu. Kanuni ya 11(b) inarejea Kanuni ya 11(1) (c). **<u>Tatizo</u>** Kanuni ya 11(1) (c) inayorejewa haipo katika Kanuni hizi. Hali hii inaleta mkanganyiko wakati wa usomaji wa Kanuni hizi.	3. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kurejea kuweka rejea sahihi.	3. Marekebisho yamefanyika katika **Kanuni ya 11** kwa kufuta rejea ya aya (c)	3. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 16 Agosti, 2024 (TS. Na. 25)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
3.	Kanuni za Mazingira ya kazi,2023 (Zimetungwa chini ya kifungu cha 109) **(TS Na. 289)** 7 Aprili, 2023	1. **Kanuni ya 4(1)** inarejea Kanuni ya 4(2) kwa kuitaja yote. **<u>Tatizo</u>** Maudhui ya Kanuni ya 4(1) yanajirudia katika Kanuni ya 4(2) 2. **Kanuni ya 4(2)** inaweka sharti kwa mwajiri kutomruhusu mfanyakazi kufanya kazi katika mazingira ya jokofu ambapo kipimo cha hali ya joto ya balbu kavu iko chini ya nyuzi joto 0. **<u>Tatizo</u>** Kanuni haijataja iwapo kipimo cha nyuzi joto kilichokusudiwa ni nyuzi joto sifuri	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa maudhui yanayojirudia. 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kipimo kinachokusudiwa ni sentigredi	1. Marekebisho ya Kanuni ya 4 yamefanyika kwa kuifuta Kanuni (2) inayojirudia na kuiandika upya. 2. Marekebisho ya **Kanuni ya 4(2)** yamefanyika kwa kuweka kipimo cha sentigredi 6	1. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 16 Agosti, 2024 (TS. Na. 24) 2. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 16 Agosti, 2024 (TS. Na. 24)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		sentigredi au nyuzi joto farenheiti 3. **Kanuni ya 9** inahusu kiwango cha kelele kinachohitajika mahala pa kazi kuwa ni 85 dB (A). **<u>Tatizo</u>** Kipimo cha kelele kwa kina makosa ya aundishi kwa kuweka mabano katika herufi A.	3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuandika Kanuni kwa usahihi	3. Marekebisho yamefanyika katika Kanuni ya 2 kwa kufuta kifupisho cha "(dBA)" na badala yake kuweka "dB(A)"	3. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 16 Agosti, 2024 (TS. Na. 24)
WIZARA YA UCHUKUZI					
4.	*The Merchant Shipping (Medical Examinations) Regulations, 2023* (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 157)	1. **Kanuni ya 5 (c)** inaweka sababu ya kufutwa ama kusitishwa kwa uteuzi pale ambapo kwa maoni ya TASAC na mazingira yanalazimu kusitisha au kufuta uteuzi.	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuifuta Kanuni ya 5(c)	1. Marekebisho yamefanyika kwa kuifuta Kanuni ya 5(c).	1. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 396)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	(TS Na. 327) 5 Mei 2023	**<u>Tatizo</u>** Hali hiyo: - a) Ni kinyume na misingi ya uandishi wa Kanuni, ambazo zinapaswa kutoa ufafanuzi zaidi wa masharti yaliyowekwa na Sheria Mama. b) Inaweza kusababisha matumizi mabaya ya Madaraka yaliyotolewa na Kanuni hizo 2. **Kanuni ya 21** inaweka utaratibu wa kushughulikia malalamiko ya baharia ama nahodha ambaye	2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha hatua inayoweza kufuatwa na mtu ambaye	2. Marekebisho yamefanyika kwa kuifuta kanuni ya 21(3) Kanuni imeboreshwa kwa kufuta Kanuni ya	2. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		hajaridhishwa na uamuzi, ambapo anaweza kuiomba TASAC ifanye mapitio ya uamuzi uliotolewa dhidi yake. **Kanuni ya 21 (3)** inaweka utaratibu wa TASAC ili kushughulikia malalamiko na kufikisha uamuzi wake kwa mlalamikaji ndani ya siku 14 tangu muda mabao malalamiko yalipokelewa. **<u>Tatizo</u>** Kanuni hailezi hatua inayoweza kufuatwa na mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa baada ya mapitio. Hali ni inaweza sababisha mkanganyiko kuhusu	hajaridhishwa na uamuzi wa baada ya mapitio.	21(3) na kuiandika upya kwa kurejea Kanuni inayoweka utaratibu wa kushughulikia malalamikp ambayo ni *"The Tanzania Shipping Agencies (Complaints Handling) Regulations, GN. 338 of 2018."*	tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 396)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		inayostahili kufuatwa baada ya uamuzi wa mapitio.			
5.	*The Tanzania Shipping Agencies (Cargo Security and Safety of Terminal Operations) Regulations, 2023* (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 61(2)(g) and (j)) **(TS Na. 381)** 2 Juni 2023	1. **Kanuni ya 3** inaweka tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Kanuni hizi. **<u>Tatizo la Kwanza</u>** Kanuni haijaweka tafsiri ya maneno kama vile *regulator*, *competent* na director general ambayo yametumika katika maeneo mbalimbali ndani ya Kanuni kama vile Kanuni ya 5(2), 12, 15(2), 51(4). 2. **Kanuni 5** inahusu mamlaka ya msimamizi kuruhusu	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka tafsiri ya maneno "regulator, "competent" na "director general" 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha sababu	1. Marekebisho yamefanyika katika Kanuni ya 3 kwa kuongeza tafsiri ya maneno "*competent*" na "*director*" 2. Marekebisho yamefanywa katika kanuni ya 5 kwa	1. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 394) 2. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		au kutoruhusu mtu au mzigo kuingia au kutoka katika eneo la bandari. **<u>Tatizo</u>** Kanuni haijabainisha sababu zinazoweza kusababisha mtu au mzigo kukataliwa kuingia au kutoka, badala yake Kanuni imeruhusu utashi binafsi kwa msimamizi kuweka sababu yoyote atakayoona inafaa.	zinazoweza kusababisha mtu au mzigo kukataliwa kuingia au kutoka bandarini.	kuonesha sababu ya kuzuia mzigo au mtu kuingia au kutoka bandarini.	kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 394)
		3. **Kanuni ya 20** inaweka wajibu kwa msimamizi kuhakikisha watu wanatembea katika eneno la bandari wanavaa vifaa vya usalama.	3. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta kanuni ya 20(1)(d)	3. Kanuni imeboreshwa kwa kufuta Kanuni ya 20(1)(d) ili kuondoa kushabihiana kwa maudhui.	3. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 394)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<u>Tatizo</u> Kanuni ya 20(1) (b) (d) inawasilisha ujumbe mmoja, ambapo (b) tayari imetaja matumizi ya viatu salama ambavyo si vile vinavyotajwa katika aya (d).			
		4. **Kanuni 23 (1) (b)** msimamizi atahakikisha kuwa vifaa vya kuzimia moto haviondolewi katika maeneo yake isipokuwa vitakapokuwa vikitumika wakati wa matumizi yake, wakati wa majaribio au wakati wa matenegezo.	4. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka sharti la kuweka vifaa mbadala wakati vifaa vimeondolewa kwa ajili ya matengenezo.	4. Kanuni ya 23 imefanyiwa marekebisho kwa kuongeza kivuo (*proviso*) mara baada ya Kanuni 23(1)(b) ambayo imeweka takwa la kuwa na vifaa mbadala wakati vifaa vilivyopo vinapokuwa kwenye majaribio au matengenezo.	4. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 394)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<u>Tatizo</u> Kanuni haizioneshi sharti la kuweka vifaa mbadala wakati vifaa vimeondolewa kwa ajili ya matengenezo.			
		5. **Kanuni ya 23 (4)** inaweka sharti kwamba, vali zuizi (block valves) zinapaswa kuwa wazi muda wote. **<u>Tatizo</u>** Masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 23 (4) hayana uhalisia.	5. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno "*kept open*" na badala yake kuweka maneno "*accessible and readly available for use*"	5. Kanuni ya 23 imefanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno "*kept open*" yaliyopo katika kanuni ndogo ya (4) na badala yake kutumia maneno "*accessible and readly available for use*".	5. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 394)
		6. **Kanuni ya 35** inampa wajibu msimamizi kuhakikisha miundombinu ipo katika ubora na mazingira mazuri.	6. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kurejea Kanuni ya 33 na 34 ili kuondoa makosa ya kiuandishi	6. Kanuni imerekebishwa kwa kurejea kanuni sahihi ambazo ni kanuni ya 33 na 34.	6. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<u>Tatizo</u> Kanuni ina makosa ya uandishi kwa kufanya rejea ya Kanuni ya 35, hali hiyo inaleta changamoto ya usomaji wa kanuni.			tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 394)
		7. **Kanuni ya 55 (3)** inamtaka msimamizi pale inapotokea upotevu wa mizigo na kutoa taarifa, kutoa taarifa kwa shirika na kufanya uchunguzi wa awali na kutoa taarifa ya uchunguzi. **<u>Tatizo</u>** Kanuni inaweka sharti kwa msimamizi kutoa taarifa ya uchunguzi badala ya kutoa taarifa ya uchunguzi wa awali.	7. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha kuwa unaokusudiwa ni uchunguzi wa awali.	7. Kanuni imeboreshwa kwa kuongeza maneno "preliminary" kati ya neno "*produce*" na neno "investigation" kwenye kanuni ya 55(3).	7. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 394)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		8. Kanuni ina makosa ya uandishi wa namba za vifungu, ambapo imeruka Kanuni ya 58. **<u>Tatizo</u>** Kurukwa kwa Kanuni hiyo kunaweza kuwa ni: - a) makosa ya kiuandishi; au b) Kutokuwekwa kwa Kanuni iliyokusudiwa. Mambo hayo yanaweza weza kusababisha kutokutimia kwa malengo yaliyokusudiwa.	8. Kanuni ifanyiwe mareklbisho kwa kuweka mpangilio sahihi wa namba za vifungu.	8. Kanuni imeboreshwa kwa kuweka mpangilio sahihi wa namba.	8. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 394)
		9. **Kanuni ya 57** inaweka adhabu ya jumla pale ambapo	9. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuendana na	9. Kanuni ya 57 imeboreshwa kwa kufuta maneno	9. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		hakuna adhabu iliyotamkwa kwa kuvunja masharti yaliyopo katika Kanuni, kuwa ni adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni ishirini ama kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano ama adhabu zote kwa pamoja. **<u>Tatizo</u>** Adhabu ya jumla inayotamkwa na kanuni hii ni kinyume na adhabu iliyowekwa na sheria mama chini ya kifungu cha 56 kinachoweka adhabu ya jumla kwa makosa	masharti ya adhabu yanyowekwa na kifungu cha 56 cha sheria mama.	"two", "twenty" na "one year" na badala yake kuweka maneno "twenty", "fourty" na "two years" mtawalia.	kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 394)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		ambayo hayajawekewa adhabu. Kifungu hiko kinataja adhabu ya faini isiyopungua shilingi za kitanzania milioni ishirini na isiyozidi shilingi milioni arobaini au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano ama adhabu zote kwa pamoja. Hali hiyo inasababisha mashaka kuhusu kuzingatiwa kwa masharti ya kifungu cha 36 (6) cha sheria ya tafsiri ya sheria kuhusu masharti ya kuweka adhabu katika sheria ndogo.			
6.	*The Tanzania Shipping Agencies*	1. **Kanuni ya 6(2)** inaipa TASAC sharti la hiari ya kutoa cheti cha usajili	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la	1. Kanuni imeboreshwa kwa kufuta neno "may"	1. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	(Shippers Registration) Regulations, 2023 (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 12(1)(k) and 61) **(TS Na. 382)** 2 Juni 2023	kwa muombaji aliyetimiza masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria. **<u>Tatizo</u>** Kanuni imeweka sharti la hiari kwa TASAC kumpatia cheti muombaji aliyetimiza masharti, badala ya kuweka sharti la lazima	lazima kwa TASAC ili kumpatia cheti muombaji aliyetimiza masharti.	badala yake kuweka neno "shall".	kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 397)
		2. **Kanuni ya 11 (1) (b)** inamtaka muombaji wa nakala rudufu ya cheti kilichopotea ama kuharibiwa, kuambatisha maombi yake na hati uthibitisho wa polisi ya upotevu na nyaraka nyingine yoyote kama itakavyohitajika na Shirika.	2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa maneno "nyaraka nyingine yoyote kama itakavyohitajika na TASAC"	2. Kanuni imeboreshwa kwa kufuta maneno "*and any other relevant document as may be required by the Corporation*".	2. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 397)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<u>Tatizo</u> **Kanuni ya 11 (b)** inalipa Shirika nguvu ya kutaka nyaraka nyingine yoyote bila kutaja nyaraka hizo. Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa.			
		3. **Kanuni ya 19 (3)** inaoesha masauala ambayo yatazingatiwa ili kuonesha kwamba, notisi imefikishwa kwa mlengwa. **<u>Tatizo</u>** Kanuni ina makosa ya uandishi kwa kurejea i aya (a) na (b) mara mbili. Hali hiyo inaleta changamoto ya	3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka mpangilio wa vifungu.	3. Kanuni imeboreshwa kwa kuweka sawa mpangilio wa aya.	3. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 397)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		usomaji na namna ya kufanya rejea.			
		4. Kanuni imerejea kuanzishwa chini ya **kifungu cha 12 (1) (k) na 61**. **<u>Tatizo</u>** **Kifungu cha 12 (1) (k)** kilichorejewa hakihusiani na mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni. Hali hii inakanganya chimbuko la mamlaka ya kutungwa kwa kanuni hizi.	4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa Kanuni ya 12(1) (k) ambayo haihusiani na mamlaka ya Waziri ya kutunga Kanuni.	4. Kanuni imeboreshwa kwa kuondoa rejea ya kifungu cha **12(1)(k)**.	4. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 397)
		5. Kanuni zina makosa ya uandishi katika mpangilio wa vifungu. **<u>Tatizo</u>** Kanuni ya 4 imetokea mara mbili ikiwa na	5. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka mpangilio sahihi wa namba za vifungu.	5. Kanuni imeboreshwa kwa kuweka mpangilio sahihi wa namba.	5. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 397)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		maudhui yanayotofautiana. Athari yake ni: - a) Inaleta mkanganyiko katika rejea ya Kanuni; na b) Inatatiza ufafanuzi wa masharti ya sheria mama.			
		6. **Kanuni ya 4 (2)** inataja matakwa ya kuzingatiwa wakati wa kuomba usajili wa wasafirishaji kwa njia ya maji. **Kanuni ya 4(2) (a) (iv)** inataja nyaraka zingine zozote kama zitavyohitajika na TASAC. **<u>Tatizo</u>** **Kanuni ya 4 (2) (a) (iv)** inaipa TASAC nguvu	6. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa uwezo wa TASAC kutaka nyaraka nyingine yoyote.	6. Kanuni imerekebishwa katika kanuni ya 4(2)(a)(iv) kwa kufuta maneno "*and any other document as may be required by the Corporation*".	6. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 397)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		ya kutaka nyaraka nyingine yoyote bila kutaja nyaraka hizo. Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa.			
		7. **Kanuni ya 4 (2) (b) (iv)** inazungumzia vigezo vya usajili wa wasafirishaji kwa njia ya Maji kwa upande wa Taasisi na Mtu binafsi. **<u>Tatizo</u>** Kanuni haitaji nyaraka zilizokusudiwa. Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa	7. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa uwezo wa TASAC kutaka nyaraka nyingine yoyote.	7. Kanuni imerekebishwa katika kanuni ya 4(2)(b)(iv) kwa kufuta maneno "*and any other document as may be required by the Corporation*".	7. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 397)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		8. **Kanuni ya 6 (3)** inazungumzia utaratibu wa TASAC kutoa notisi iwapo imekataa maombi ya usajili. **<u>Tatizo</u>** Kanuni haioneshi muda mahsusi ambao Notisi itapaswa kutolewa tangu TASAC kupokea maombi hayo. Hali hii:- a) Inaweka utata kuhusu muda wa kusubiria notisi; b) Inaikosesha TASAC mwongozo kuhusu muda wa kutoa notisi.	8. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha muda mahsusi ambao Notisi itapaswa kutolewa tangu TASAC kupokea maombi ya usajili.	8. Kanuni imerekebishwa katika kanuni ya 6(3) kwa kuainisha muda mahsusi wa kutoa notisi.	8. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 397)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		9. **Kanuni ya 16 (2)** inaweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na elfu hamsini na isiyozidi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote kwa pamoja. **<u>Tatizo</u>** Adhabu hiyo imevuka ukomo wa sheria za nchi. Hali hiyo inasababisha mashaka kuhusu kuzingatiwa kwa masharti ya kifungu cha 36 (6) cha sheria ya tafsiri ya sheria kuhusu masharti ya kuweka adhabu katika sheria ndogo.	9. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuendana na adhabu zilizowekwa kwatika sheria mama.	9. Kanuni imeboreshwa katika kanuni ya 16(2) kwa kufuta maneno "two hundred and fifty thousand", "one million", "six months" na "one year"na badala yake kuweka maneno "twenty thousand", fourty million", "one year" na "five years"	9. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 397)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		10. Kanuni ina Majedwali saba yanayotoa ufafanuzi wa Kanuni mbalimbali **<u>Tatizo</u>** Majedwali yana makosa ya uandishi kwa kurejea Kanuni zinazoyaanzisha ambazo si sahihi	10. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kurejea kanuni sahihi zinazoanzisha majedwali.	10. Kanuni imefanyiwa marekebisho kwa kufanya marejeo ya kanuni sahihi zilizoanzisha Majedwali.	10. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 397)
7.	Kanuni za Usajili wa Wasafirishaji kwa njia ya Maji, 2023 **(TS Na. 384 la 2023)** 2 Juni 2023	**Kanuni ya 12** inaweka utaratibu wa Msafirishaji kuomba nakala iliyodurufiwa ya Cheti chake alichopoteza. Kanuni ya 12 (b) inamtaka muombaji kuambatisha maombi hayo pamoja na nakala ya taarifa ya upotevu na nyaraka nyingine yoyote kama itakavyohitajika na TASAC.	Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la TASAC kuomba nyaraka nyingine yoyote.	Kanuni imeboreshwa kwa kufuta maneno "*na nyaraka nyingine yoyote kama itakavyohitajika*".	Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 408)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<u>Tatizo</u> Kanuni haitaji nyaraka zilizokusudiwa. Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika kwa nyaraka halisi zinazokusudiwa			
8.	Kanuni za Ulinzi wa Mizigo na Usalama Katika Utendaji Kazi wa Bandari na Bandari Kavu, 2023 (Zimetungwa chini ya kifungu cha 5 (b), (c), (d) na 61(2) (g), (j)) **(TS Na. 387)** 2 Juni 2023	1. Kanuni imetumia neno "bila kujali" katika maeneo mbalimbali. **<u>Tatizo</u>** Matumizi ya neno bila kujali yanaondoa maana iliyokusudiwa katika masharti yaliyowekwa na sheria ndogo. 2. **Kanuni ya 12** inazungumzia mizigo iliyopigwa marufuku bandarini na inaelezewa kuanzia sehemu (a) mpaka	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno "bila kujali" na badala yake kuweka maneno "bila kuathiri" 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari ya kiuandishi	1. Kanuni imeboreshwa kwa kufuta maneno "bila ya kujali" na kuweka maneno "bila ya kuathiri". 2. Kanuni imeboreshwa katika kanuni ya 12 (a) kwa kufuta neno "hauwezi" na badala yake	1. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 406) 2. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		sehemu (d). Sehemu (a) inazungumzia mzigo usioruhusiwa iwapo umeshambuliwa, wenye sumu kali, kuoza au kuharibiwa na ukungu na hauwezi kuharibika ukiwa ndani ya bandari au bandari kavu. **<u>Tatizo la Kwanza</u>** Tatizo la kimaandishi baada ya kutumia neno "unaweza kuharibika'' imeandikwa ''hauwezi kuharibika'' hali hii inaweza kuathiri lengo lililokusudiwa na sheria mama.		kuweka neno "kuweza"	tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 406)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<u>Tatizo la Pili</u> Kanuni imetua neno umeshambuliwa pasipo kulifafanu. Hali hiyo inaleta mkanganyiko wa maana iliyokusudiwa.			
		3. **Kanuni ya 14 (4)** inaelekeza utaratibu wa namna ya kushusha na mizigo hatarishi bandarini. **<u>Tatizo</u>** Kanuni zimetaja lori kama chombo cha kupokea mzigo hatarishi kutoka katika meli. Hii inasababisha kutokutambulika kwa vyombo vingine vinavyotumika kupakia mizigo bandarini	3. Kanuni ya 14(4) ifanyiwe marekebisho ili kuongeza vyombo vingine vya usafirishaji.	3. Kanuni ya 14(4) imeboreshwa kwa kuongeza maneno "na behewa" katikati ya maneno "lori" na "na"	3. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 406)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		4. **Kanuni ya 53 (2)** inahusu mafunzo ya rejea na endelevu kwa afisa ulinzi **<u>Tatizo</u>** Kanuni haijafafanua kwamba mafunzo yatakayotolewa yatahusiana na fani inayohusika.	4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha mafunzo yatakayotolewa yatahusiana na fani inayohusika	4. Kanuni ya 53(2) imeboreshwa kwa kuongeza maneno *"kuhusiana na ulinzi na usalama"* kati ya neno *"mafunzo"* na *"ya"* ili kufafanua mafunzo.	4. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 406)
9.	*The Merchant Shipping (Establishment and Operation of Aids to Navigation) Regulations, 2023* (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 217 na 222) **(TS Na. 482)** 21 Julai 2023	1. **Kanuni ya 3** inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali. **<u>Tatizo</u>** Kanuni ina makosa ya kiuandishi kwa kutofuata mpangilio wa maneno katika mtiririko wa kialfabeti. 2. **Kanuni ya 19** inahusu utatuzi wa migogoro inayohusu malipo ya madeni.	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari za kiuandishi 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha utaratibu	1. Kanuni ya 3 imefanyiwa marekebisho kwa kuweka mpangilio wa maneno katika mtiririko wa kialfabeti. 2. Kanuni ya 19 imefanyiwa marekebisho kwa kuainisha utaratibu	1. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 395) 2. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
			wa kusikiliza malalamiko.	wa namna ya usikilizwaji wa malalamiko kama iliyoainishwa katika Kanuni za Kushughulikia Malalamiko, Tangazo la Serikali *Na. 338 la mwaka 2018.*	Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 395)
		<u>Tatizo</u> Kanuni inaelekeza migogoro ya namna hiyo isikilizwe na kuamuliwa na mahakama pasipo kuweka mfumo mwingine wa kusikiliza mashauri kabla ya kufika mahakamani.			
		3. **Kanuni ya 21** inampa Waziri mamlaka ya kutoa msamaha wa gharama yote au sehemu kwa vifaa vya kuongozea meli **<u>Tatizo</u>** Kanuni haijaonesha vigezo ambavyo Waziri atazingatia ili kutoa msamaha. Kutokuwekwa kwa vigezo, utoaji wa	3. Kanuni ifanyie marekebisho ili kuainisha vigezo vitakavyozingatiwa na Waziri ili kutoa msamaha.	3. Kanuni ya 21 imefanyiwa marekebsho kwa kumpa mamlaka Msajili kutoa msamaha kwa meli ambazo zimepata msamaha kutoka kwa mtoa huduma za vifaa vya kuongozea meli kutolipa tozo za matumizi ya vifaa vya kuongozea meli.	3. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 395)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		misahama isiyo na muongozo. 4. **Kanuni ya 26** inazungumzia ulinzi dhidi ya matendo yaliyofanywa na TASAC ama afisa wa TASAC katika uwajibikaji chini ya kanuni hizi kwa kigezo cha matendo hayo kufanyika kwa nia njema. **<u>Tatizo</u>** Kanuni inaweka sharti la kuondoa uwajibikaji kwa upande wa TASAC ama afisa wa TASAC kwenye matendo yaliyoonekana kufanyika kwa nia njema.	4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kufuta Kanuni ya 26.	4. Kanuni zimefanyiwa marekebisho kwa kufuta kanuni ya 26.	4. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS. Na. 395)

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		Hali hii ni kinyume na misingi ya haki.			
WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI					
10.	Kanuni Za Ukusanyaji Na Uchakataji Wa Taarifa Binafsi,2023 (Zimetungwa chini ya kifungu cha 64) **(TS Na. 349)** 12 Mei 2023	1. **Kanuni ya 4(3)(c)** inataja moja ya sharti la kuzingatiwa wakati wa kuchakata maombi ya usajili wa ukusanyaji na uchakataji wa Taarifa binafsi **<u>Tatizo</u>** Kanuni ya 4(3) (c) inataja sharti la kuwasilisha nyaraka nyingine yoyote kama Tume itakavyohitaji wakati kuomba usajili wa ukusanyaji na uchakataji wa Taarifa binafsi.	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la Tume kuhitaji nyaraka nyingine yoyote.	1. Marekebisho ya Kanuni ya 4(3)(c) yamefanyika kwa kuifuta aya (c) na badala yake kuiandika "taarifa nyingine yoyote kama tume itakavyo hitaji baada ya kupokea maombi"	1. Rasimu ya Marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		2. **Kanuni ya 9(2) (e)** inataja moja ya Taarifa za wakusanyaji na wachakataji zitazohifadhiwa katika rejista. **<u>Tatizo</u>** **Kanuni ya 9(2) (e)** inataja taarifa nyingine yoyote kama Tume itakavyoelekeza. Sharti hilo: - a) linasababisha kutotabalika taarifa zinazohitajika; na b) linaondoa mantiki ya sheria ndogo kutoa ufafanuzi unaojitosheleza kuhusu masharti ya sheria mama	2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la Tume kuhitaji taarifa nyingine yoyote.	2. Marekebisho ya Kanuni ya 9(2)(e) yamefanyika kwa kuifuta aya (e) na badala yake kuiandika "taarifa nyingine yoyote kama Tume itakavyoelekeza kwa kuzingatia mahitaji ya wakati husika"	2. Rasimu ya Marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		3. **Kanuni ya 20 (2)** inahusu maombi ya kibali cha kusafirisha taarifa binafsi nje ya nchi. **<u>Tatizo</u>** **Kanuni ya 20(2)(i)** inaweka kigezo kwa muomba kibali kuwasilisha taarifa nyingine yoyote kama itakavyohitajika na Tume. Sharti hilo: - a) linasababisha kutotabalika taarifa zinazohitajika; na b) linaondoa mantiki ya sheria ndogo kutoa ufafanuzi unaojitosheleza kuhusu masharti ya sheria mama.	3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la Tume kuhitaji taarifa nyingine yoyote.	3. Marekebisho ya Kanuni ya 20(2) yamefanyika kwa kukifuta kifungu kidogo cha (2) na badala yake kuiandika "taarifa nyingine yoyote kama tume itakavyo hitaji baada ya kupokea maombi"	3. Rasimu ya Marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		4. **Kanuni ya 27** inaweka msingi wa mambo muhimu ya kuzingatiwa na mkusanyaji ama mchakataji wa Taarifa Binafsi. Sehemu (i) inaweka msingi wa kulinda taarifa binafsi nyeti kwa hatua za kutosha na ikiwezekana kuhifadhi taarifa hizo tofauti na zinapohifahdhiwa taarifa binafsi nyingine. **<u>Tatizo</u>** Kanuni haijaweka sharti la lazima la kuhifadhi taarifa binafsi nyeti tofauti na taarifa binafsi za aina nyingine. Hali hii inaweza kufifisha lengo	4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la lazima la kuhifadhi taarifa binafsi nyeti tofauti na taarifa binafsi za aina nyingine.	4. Kanuni ya 27 imefanyiwa marekebisho kwa kuonesha taarifa binafsi nyeti zitahifadhiwa sehemu tofauti na zinapohifadhiwa taarifa nyingine binafsi".	4. Rasimu ya Marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		lililowekwa na Sheria mama katika ulinzi wa taarifa binafsi.			
11.	Kanuni za Taratibu za Kushughulikia Malalamiko ya Ukiukwaji wa Misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, 2023 **(TS Na. 350)** 12 Mei 2023	1. **Kanuni ya 4(3)** inaelezea utaratibu wa kuwasilisha malalamiko ya mtu au kikundi kuhusu ukiukaji wa ulinzi wa Taarifa binafsi au kutoridhishwa na uamuzi wa mkusanyaji au mchakataji kuhusiana na taarifa binafsi. **<u>Tatizo</u>** Kanuni imetambua utaratibu wa kupokea malalamiko ya kikundi ilhali Kanuni hazitambui malalamiko ya kikundi.	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka utaratibu wa kuwasilisha malalamiko ya kikundi	1. Marekebisho ya Kanuni yamefanyika kwa kuifuta **Kanuni ndogo (1)** na kuiandika upya ili kuonesha utaratibu wa upokeaji wa malalamiko ya kikundi.	1. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS Na. 407).

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		2. **Kanuni ya 4(5)** inazungumzia utaratibu wa Tume kupitia malalamiko ili kujiridhisha usahihi wake na uzingatiaji wa sheria ili Tume iweze amua kuruhusu kupokea malalamiko ama vinginevyo. **<u>Tatizo la kwanza</u>** Kanuni haioneshi muda ambao Tume itatumia kujiridhisha na usahihi wa malalamiko tangu kuyapokea. Hali hii inaweza kuleta changamoto ya ucheleweshaji wa Haki ya mlalamikaji na kuendeleza madhara anayoyalalamikia	2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha muda ambao Tume itatumia kujiridhisha na usahihi wa malalamiko tangu kuyapokea.	2. Marekebisho ya **Kanuni ya 4(5)** yamefanyika kwa kuweka muda wa siku Tano ambao Tume itatumia kujiridhisha na usahihi wa malalamiko tangu kuyapokea.	2. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS Na. 407).

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<u>Tatizo la Pili</u> Kanuni hazioneshi muda ambao malalamikaji atapaswa kuwa amefikisha malalamiko yake kwa Tume tangu muda ambao uamuzi wa mtunza taarifa ama mchakata taarifa unaolalamikiwa umetokea. Hali hii ni kinyume na kanuni za upatikanai wa haki na uchakataji wa malalamiko.			
		3. **Kanuni ya 8** inamtaka mlalamikaji kuandaa na kuwasilisha kwa Tume majibu dhidi ya Utetezi wa mlalamikiwa ndani ya muda uliotolewa	3. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka muda ambao mlalamikaji atapaswa kutumia kuandaa majibu dhidi ya utetezi wa malalamikiwa.	3. Marekebisho ya **Kanuni ya 8** yamefanyika kwa kuweka muda wa siku saba ambao mlalamikaji atapaswa kutumia kuandaa majibu	3. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS Na. 407).

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		baada ya kupokea utetezi. **<u>Tatizo</u>** Kanuni haioneshi muda ambao mlalamikaji atapewa ili kuandaa majibu dhidi ya utetezi wa mlalamikiwa. Hali hii inaweza kurefusha muda wa uchakataji wa malalamiko hivyo, kuathiri upatikanaji wa haki kwa wakati. 4. **Kanuni ya 12 (3)** inazungumzia utaratibu wa kufuatwa mara baada mlalamikaji au mlalamikiwa kuruhusiwa kufanya marekebisho ya	4. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka muda mahsusi atakaopewa muombaji kwa ajili ya kufanya marekebisho.	dhidi ya utetezi wa malalamikiwa. 4. Marekebisho ya **Kanuni ya 12 (3)** yamefanyika kwa kuweka muda wa usiozidi siku saba ili muombaji aweze kufanya marekebisho ya malalamiko, utetezi au majibu.	4. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Mei, 2024 (TS Na. 407).

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		malalamiko, utetezi au majibu. **<u>Tatizo</u>** Kanuni haioneshi muda ambao Tume itampa mwombaji wa kibali kufanya marekebisho yanayohusika, jambo linaloweza kusababisha: - a) Mhusika kutumia muda mrefu kufanya marekebisho na kuchelewesha haki kwa upande mwingine; b) Kukosekana kwa mwongozo kuhusu muda wa kufanya marekebisho na kuathiri uthabiti wa			

Na	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
